# Nipashe

Jumamosi Desemba 26, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580441

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




**Lissu** awataka wana CHADEMA kutokukata tamaa



UKURASA 4

**Askari** wawili wa JWTZ wafa ajali ya pikipiki

UKURASA 4

**Pochettino anukia kubeba mikoba PSG**

UKURASA 20

# Maaskofu watoa kauli nzito ibada za Krismasi

UKURASA 2

## YALIYOMO


UKURASA WA 5

**WATOTO SABA WAANGUKIWA NA UKUTA WA NYUMBA**

WATOTO saba wa Mtaa wa Stoo, Kata ya Igunga Mjini, akiwamo...

UKURASA WA 5

**WAZIRI AAMURU KUKAMATWA KWA WATOROSHAJI MADINI**

WAZIRI wa Madini, Doto Biteko, ameamuru kukamatwa kwa...

UKURASA WA 9

**ASKOFU ATAKA VYAMA VYA SIASA VISAKE MWAFAKA**

ASKOFU wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Kati, Dk. Dikson...




**Askofu Shao**
" Hatua ya wapinzani imeleta amani Zanzibar".



**Askofu Kinyunyu**
"Mungu ametukinga na corona"



**Askofu Isaac Amani**
"Acheni kuuza watoto kwa tamaa za utajiri"



**Askofu Sangu**
"Watanzania tusiichezee amani"



**Askofu Sehaba**
"Malalamiko ya uchaguzi yafanyiwe kazi"



**Askofu Masangwa**
"Tuzalishe na kutumia bidhaa za ndani"

## Magufuli asisitiza Watanzania kumshukuru Mungu

UKURASA 4

## Jengo la kihistoria laporomoka Zanzibar

UKURASA 4




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



**MICHEZO** STRAIKA MPYA KUIPAISHA YANGA UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Maaskofu watoa kauli nzito Krismasi

**Na Waandishi Wetu**

MAASKOFU wa makanisa mbalimbali ya kikristo nchini, jana, walitoa kauli mbalimbali huku wengi wakitaka watu waliopewa mamlaka katika nafasi mbalimbali serikalini kutenda haki na kudumisha amani.

Sambamba na hilo, pia wamewapongeza wapinzani visiwani Zanzibar kukaa meza ya mazungumzo na serikali hatua ambayo imewezesha kurejesha amani iliyokuwa katika hali tete na hatimaye kuundwa tena kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK).

Kauli hizo walizotoa katika ibada za Krismasi zilizofanyika kwenye makanisa hayo, ikiwa ni kumbukumbu ya kuzaliwa kwa Mwokozi Yesu Kristo zaidi ya miaka 2,000 iliyopita.

Vilevile walitaka Watanzania kuendelea kudumisha amani pamoja na kufanya kazi kwa ajili ya kujiletea maendeleo.

Kuhusu uchaguzi mkuu uliopita, maaskofu hao walisema Watanzania wanapaswa kuacha kunung'unika huku wakiitaka serikali na vyama vya siasa kusahau yaliyopita na kuungana kuijenga Tanzania. Pia waliitaka serikali kufanyia kazi kasoro zilizojitokeza wakati wa uchaguzi.

Akizungumza katika ibada iliyofanyika Kanisa Kuu la Katoliki mjini Zanzibar, Askofu wa kanisa hilo, Jimbo la Zanzibar, Augustino Shao, alisema licha ya udhaifu uliojitokeza, kitendo cha wapinzani kuingia katika SUK kimeleta amani na kimejenga uwanja wa mazungumzo katika kuondoa tofauti zilizopo.

Katika sehemu ya mahubiri yake, Askofu Shao alimpongeza Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, kwa kufanya mazungumzo na upinzani hasa Chama cha ACT-Wazalendo hatua ambayo alisema imeleta matumaini katika kuondoa tofauti na itikadi za kisiasa.

"Mungu Emmanuel ni nguvu na mwanga katika giza ndiyo maana katika kumbukumbu ya ujio wake, anaagiza tuwe mwanga wa kuondoa giza la maovu na uvunjwaji wa haki iliyo msingi wa amani," alisema. Aliongeza kuwa: Emmanuel Mungu pamoja nasi anatuagiza tudumishe haki na amani kwa kuheshimu utu wa kila raia na kuwa tayari kwa mazungumzo pale mitazamo yetu ya kijamii na kisiasa inapotofautiana."

Kwa mujibu wa Askofu Shao, Tanzania imekuwa kioo cha amani kwa sababu ya kuheshimu utu wa kila mtu na haki za msingi za watu wote na siasa safi imeipa heshima nchi. Askofu huyo alisema vifo vya raia Tanzania Bara na Zanzibar katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu ni ishara tosha kwamba haijafahamika maana ya demokrasia licha ya kutofautiana, lakini bado ni wamoja.

"Mungu anatuasa tuwe watu wa amani kwa mazungumzo zaidi, ubabe katika siasa ni maumivu ya wengi na huleta vifo," alisema.

Alisema ili kujenga haki, amani na maisha bora kila mmoja ahusike na mabadiliko ya maendeleo kwa sababu anayofanya Rais Dk. Mwinyi pamoja na wasaidizi wake aliowateua yanatia moyo.

"Angalau sasa tunaona kukemewa kwa wale wachache waliodhani kwamba kisiwa hiki ni mali yao, sasa wanaelimishwa kwamba hakuna aliye juu ya sheria na kuwa raia wote wana haki sawa," alisema.

Hata hivyo, alisema lazima kuwe na nguvu za ziada kukemea na kuwawajibisha wala rushwa na mafisadi na hatua za Dk. Mwinyi katika hilo zinaleta matumaini kwamba yajayo ni neema tupu.

Askofu Shao alisema Rais Dk. Mwinyi amesema hataki kufufua makaburi, lakini kwa mantiki ya dini zote aliyeiba na kuhodhi mali za serikali ni lazima arudishe na hatua za kisheria zichukuliwe.

## Kinyunyu: Tumshukuru Mungu kutukinga corona

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

ASKOFU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Dodoma, Amon Kinyunyu, amewataka Watanzania kumshukuru Mungu kwa kuwakinga dhidi ya ugonjwa wa corona pamoja na kuwajalia amani iliyopo.

Pia amewataka wananchi wote kuendelea kuilinda na kuidumisha amani ili kila mtu apate nafasi ya kufanya kazi za kukuza uchumi wake na taifa kwa ujumla.

Askofu Kinyunyu alisema hayo wakati wa mahubiri ya ibada ya krismasi iliyofanyika katika Kanisa Kuu Usharika wa Dodoma Mjini, jijini hapa. Alisema Watanzania wanatakiwa kumshukuru Mungu kwa kuvuka katika kipindi kigumu cha ugonjwa wa corona ambao umeendelea kuisumbua dunia na kuua watu wengi.

"Hapa sisi tunamshukuru Mungu ni wazima na tupo kwenye ibada ya sikukuu ya Krismasi tukikaa hivyo na kuabudu. Mataifa mengine leo hii wameshindwa hata kukusanyika hivi. Hivyo tunakila sababu ya kumshukuru huyu Mungu kwa kuendelea kutukinga na corona," alisema.

Krismasi, alisema maana yake ni kumbukumbu ya kuzaliwa kwa Yesu Kristo zaidi ya miaka 2,000 iliyopita ambaye alizaliwa kwa ajili ya kuwakomboa wanadamu na dhambi zao.

Kutokana na hali hiyo, Askofu Kinyanyu Krismasi iwe sababu ya watu kukaa pamoja na kupatana kwa sababu Yesu alikuja ili kuleta amani kwa makundi yote. Katika kusherehekea sikukuu hiyo, aliwataka watu wote bila kujali imani zao, kushirikiana ili kudumisha amini iliyopo.

Pia, aliwataka wazazi kukaa na familia zao na kushiriki chakula kwa pamoja ili kujenga upendo ambao ndio lengo lingine la kumbukumbu hiyo ya sikukuu ya kuzaliwa kwa Yesu Kristo.



Rais Dk. John Magufuli akishiriki Misa Takatifu ya Krismasi katika Kanisa la Bikira Maria Imakulata, Ikulu Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

## Askofu akemea kuuza watoto kupata utajiri

**Na Daniel Sabuni,** ARUSHA

ASKOFU Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Arusha, Isaac Amani, amewataka baadhi ya waumini wenye imani za kishirikiana kuacha tabia ya ukatili wa kuuza watoto wadogo kama kuku kwa ajili ya kujipatia utajiri.

Badala yake, Askofu Mkuu Amani amewataka watu hao watubu na kumrudia Mungu ili Yesu azaliwe katika mioyo yao.

Pia amewataka wazazi hasa wa kiume kuacha mara moja tabia ya kuwabaka, kuwapiga na kuwanyanyasa watoto kwa imani hizo hizo kwa kuwa husababisha makovu na maumivu kwenye mioyo kwenye jamii na watoto wenyewe.

Akizungumza wakati wa ibada ya Krismasi jana iliyofanyika katika Kanisa la Mtakatifu Teresia wa Mtoto Yesu, jijjni hapa, alisema kumekuwapo na tabia za baadhi ya watu wanaoogea maji yaliyooshea maiti kwa imani pia ya kujipatia utajiri kupitia biashara zao.

Askofu Amani alisema kuna baadhi ya Watanzania ambao wengine ni Wakristo wenye tabia ya kufanya biashara ya watoto wadogo kwa lengo la kujipatia utajiri jambo ambalo alilikemea na kuliita kuwa ni ukatili uliopitiliza ambao huharibu upendo wa jamii na taifa zima.

"Nani amekuambia kuuza mwanadamu kunaleta utajiri? Kuoga maji yaliyooshea maiti ni utajiri? Jambo hili linaumiza sana. Tumesikia kwenye vyombo vya habari watoto wanauzwa hospitalini wanapozaliwa,

mitaani wanapotea na baadaye tunasikia wameuawa tena baada ya kubakwa. Mrudieni Mungu ambaye amemtuma mwanawe Yesu Kristo aliyezaliwa atukomboe," alisema.

Alisema wazazi hasa wa kiume wapunguze ubabe, udikteta na manyanyaso kwenye familia dhidi ya watoto na badala yake wawalee wakiwaonyesha mfano wa amani na upendo katika ndoa ili kujenga taifa lenye upendo na amani.

"Kuna familia zingine nyingi baba akiingia ndani, watoto wanakimbia na kujificha, watoto wengine wamejeruhiwa kwa kupigwa wana makovu miilini mwao na mioyoni. Tuache ukatili, ukifanya hivyo wakati wakiwa wamekuwa

utashangaa mtoto amempiga panga mzazi. Hayo ndio matunda mabaya ya kuwalea kwenye ukatili," alisema.

"Tuache ukatili kwa watoto ndugu zangu. Niliona jambo la kufadhaisha kwenye mitandao ya kijamii hivi karibuni, kuna mama mmoja alikuwa kitumia vibaya dawa za uzazi wa mpango. Alipata ujauzito baadaye akajaribu kutoa mimba, mtoto alipozaliwa alikuwa na pua mbili na sura

ya ajabu. Tusimpangie Mungu kwenye uumbaji," alisisitiza.

Katika hatua nyingine, Askofu Mkuu Amani alisema Jimbo Kuu Katoliki la Arusha limezindua kitabu kinachofundisha namna ya kumlea na kumlinda mtoto, lakini na fomu maalum ya za kujaza kama mkataba sehemu kama shule, makanisani na taasisi walipo watoto na watu wengine ili kuweka mkazo ulinzi wa watoto.

"Wakati mwingine wanaowazunguka watoto kama ndugu wa karibu, walimu ndio wanaoongoza kutatendea ukatili watoto. Sasa kwa fomu hizo, atakayekwenda kinyume, sheria za nchi zitachukua mkondo wake kwa aliyetia saini mkataba wa mtoto husika, hii itasaidia ulinzi wa watoto," alisema.

**NAFASI ZA SHULE**

Keland Nursery and Primary School iliyopo Salasala Rtd inatangaza Nafasi Za Awali Na Msingi. Mawasiliano : 0713327613.

HABARI KITAIFA



Jumba la kihistoria la Beitel a Jaib lililoko Mjimkongwe limeanguka jana. Linasadikiwa kuua watu waliokuwa wakilifanyia ukarabati. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Sangu aonya Watanzania kuchezea amani ya Taifa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

ASKOFU wa Kanisa Katoliki Jimbo la Shinyanga, Liberatus Sangu, amewataka Watanzania wasiichezee amani ya nchi, bali waidumishe ili waishi kwa upendo na kufanya shughuli za maendeleo.

Sangu alibainisha hayo juzi wakati akiendesha ibada ya mkesha wa Krismasi, iliyofanyika usiku kwenye Kanisa Kuu Parokia ya Ngokolo Mjini Shinyanga na kuhudhuriwa pia na Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko.

Alisema Watanzania wanapaswa kuilinda amani ambayo iliasisiwa na Rais wa Kwanza wa Tanzania, Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere na kuacha kuichezea ili kutoingia kwenye machafuko.

"Nawaonya Watanzania tusiichezee amani ya nchi yetu. Bila amani hakuna upendo, furaha, wala maendeleo. Kuna mataifa yana wivu sana na Tanzania na kuanza kutuchonganisha ili tufarakane na kuvuruga amani tuliyo nayo.

Tusikubali bali tuilinde na kuidumisha amani ambayo tuliachiwa na Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere," alisema Sangu.

Askofu Sangu aliipongeza serikali mkoani Shinyanga kwa kupunguza tatizo la mauaji ya vikongwe na kuomba kasi iongezwe zaidi ya kumaliza kabisa mauaji hayo ya watu wasio na hatia, hasa katika maeneo ya vijijini ambako bado yanaendelea.

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Mboneko, alimwahidi Askofu Sangu kuwa maombi yake yote ambayo ameyaomba kwa serikali yatatekelezwa.

Sambamba na hilo, aliwataka wananchi wawe na hofu ya Mungu na kutenda yaliyo mema na kuacha kufanya mambo maovu pamoja na kusherehekea sikukuu kwa amani na utulivu.

# Wataka kasoro za uchaguzi zirekebishwe

**Na Waandishi Wetu**

VIONGOZI wa Anglikana Dayosisi ya Morogoro na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Iringa, wamezungumzia mambo yaliyojitokeza katika uchaguzi mkuu, huku wakitaka kasoro zilizojitokeza zirekebishwe.

Kauli kuhusu mambo hayo zilitolewa na Askofu Godfrey Seheba wa Kanisa la Anglikana Morogoro na Msaidizi wa Askofu wa KKKT Dayosisi ya Iringa, Mchungaji Askari Mgeyekwa.

Askofu Seheba aliiomba serikali na viongozi wote kufanyia marekebisho baadhi ya malalamiko yaliyojitokeza wakati wa uchaguzi mkuu. Aliyasema hayo wakati wa ibada ya Krismasi iliyofanyika katika Kanisa la Utatu Mtakatifu mjini hapo.

Alisema ili amani iendelee kuwapo, viongozi wanapaswa kutenda haki kwa kila mwananchi, hivyo hata malalamiko yaliyotolewa na baadhi ya watu wakati wa uchaguzi yanatakiwa kufanyiwa marekebisho ili uchaguzi ujao yasijitokeze tena.

Kwa mujibu wa Askofu Seheba, amani ndiyo msingi bora wa maendeleo, hivyo viongozi wana wajibu wa kutenda haki na kudumisha umoja na ushirikiano ulioachwa na viongozi waliopita.

Askofu huyo aliwataka Wakristo kusherehekea sikukuu hiyo kwa kutenda mema badala ya kujihusisha na vitendo vya kihalifu ambavyo vinaleta picha mbaya kwa jamiii.

**ACHENI KUNUNG'UNIKA**

Naye Mchungaji Mgeyekwa amewataka waumini wa kanisa hilo, kuacha kuendelea kunung'unika kuhusu yaliyotokea wakati wa uchaguzi mkuu na badala yake kuungana na Rais John Magufuli kujenga nchi.

Akizungumza katika Usharika wa Kanisa Kuu Iringa Mjini wakati akitoa salamu za Krismasi kwa niaba ya Askofu wa Dayosisi hiyo, Blaston Gavile, ambaye yuko nje ya mkoa kwa matibabu, alisema kuna mambo ambayo watu hawakuridhika nayo lakini ni jambo kumshukuru Mungu kuona uchaguzi umepita salama.

Mchungaji Mgeyekwa alisema tofauti na nchi zingine ambazo uchaguzi unapofanyika amani hutoweka na machafuko hutokea, Tanzania hali ni shwari.

Alisema wajibu wa Wakristo ni kuendelea kuwa kielelezo bora kwa jamii kwa kuliombea taifa na kuona nchi inaendelea kusonga mbele zaidi.

Kwa mujibu wa Mgeyekwa, Tanzania ni nchi ambayo imekuwa tofauti na nchi zingine duniani wakati zinaendelea kuteseka na corona, hapa hakuna shaka wala hofu dhidi ya ugonjwa huo.

# Asisitiza matumizi bidhaa viwanda ndani

**Na Allan Isack,** ARUSHA

ASKOFU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Kaskazini Kati, Dk. Solomon Massangwa, amesema umefika wakati kwa Tanzania kutumia viwanda vya ndani kutengeneza na kuzalisha bidhaa zake.

Dk. Massangwa aliyasema hayo jana, katika maadhimisho ya Sikukuu ya Krismasi yaliyofanyika katika Kanisa Kuu la Dayosisi hiyo, Usharika wa Arusha Mjini. "Tunahitaji Tanzania ya aina gani au bara la Afrika linalouza malighafi kila siku inatakiwa ifike wakati tuseme imetosha hatuwezi kuuza malighafi bali kutengeneza bidhaa zetu wenyewe," alisema Massangwa.

Alisema kama Tanzania itahitaji kusonga mbele lazima itaingia kwenye hatari ya mapambano na ushindani wa kiuchumi, hivyo viongozi wanapaswa kusimama imara kikamilifu katika hatari itakayojitokeza.

"Kuzaliwa kwa Yesu Kristo, Watanzania tunatakiwa kusema imetosha kuuza malighafi nje ya nchi na badala yake tuzalishe bidhaa kamili kwa kuendeleza uchumi wa viwanda vyetu," alisema.

# Waumini wahimizwa upendo na amani

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MCHUNGAJI wa Kanisa la Anglikana la Mtakatifu Gabriel, Kibaha mkoani Pwani, Exavia Mpambichile, amewataka waumini wa kanisa hilo, kuimarisha upendo na amani ili kupata mafanikio katika nyanja mbalimbali ikiwamo kiuchumi.

Aliyasema hayo jana wakati akitoa salam za sikukuu ya Krismasi kwa waumini wa kanisa hilo, wakati wa ibada iliyofanyika kanisani hapo.

"Mafanikio yoyote yanakuja kukiwa na hali ya amani, lakini kama hakuna amani hata upendo itakuwa ni ndoto na maendeleo hayawezi kupatikana. Kupitia sikukuu hii nawaomba endeleeni kuimarisha upendo," alisema.

Mchungaji Mpambichile alisema ni vyema waumini wakajituma kufanya kazi zilizo halali, huku wakimtegemea Mungu kwa kuwa mafanikio hayaji mara moja bali kwa kujituma kwa juhudi na maarifa.

Mpambichile alisema wakati serikali inaendelea kuweka mipango mizuri ya kuhakikisha maisha ya Watanzania yanaendelea vizuri, hivyo ni vyema wananchi wakaunga mkono juhudi hizo kwa kufanya kazi.



Wakazi wa jijini Dar es Salaam wakiwa wamepanga foleni ya kununua nyama kwa ajili ya sikukuu ya Krismasi katika eneo la Ubungo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# JPM asisitiza Watanzania kumshukuru Mungu

**Na Mwandishi Maalum,** DODOMA

RAIS John Magufuli, jana, aliungana na waumini wa Kanisa Katoliki Parokia ya Bikira Maria Imakulata, Ikulu Chamwino mkoani Dodoma kusali Misa Takatifu ya Krismasi ambayo ni maadhimisho ya kuzaliwa kwa Yesu Kristo.

Baada ya misa hiyo iliyoongozwa na Paroko wa Parokia hiyo, Padre Paul Mapalala, Rais Magufuli aliwapongeza na kuwatakia heri Watanzania wote kwa sikukuu ya Krismasi na akawataka kuendelea kumshukuru Mungu kwa miujiza na upendo mkubwa anaolitendea Taifa la Tanzania.

Rais Magufuli alisema upendo na miujiza ya Mungu kwa Tanzania inajidhihirisha katika kipindi hiki, ambapo dunia inapita katika wakati mgumu wa janga la ugonjwa wa corona (Covid-19), ambapo maelfu ya watu wanaendelea kupoteza maisha kila siku, lakini Tanzania imeepushwa na janga hilo na maisha ya Watanzania yanaendelea kama kawaida.

Aliwaomba Watanzania wote waendelee kumshukuru na kumwomba Mungu aendelee kulilinda taifa lao dhidi ya ugonjwa huo, na kuwaombea wananchi wa mataifa mengine waepushwe na corona.

Rais Magufuli pia alitoa wito kwa viongozi wa mataifa mbalimbali duniani kukubali kumweka Mungu mbele katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa corona badala ya kutegemea nguvu za binadamu pekee.

Pamoja na kuwatakia heri ya Krismasi, Rais Magufuli aliwataka Watanzania kuendelea kuchapa kazi za uzalishaji mali, ili kuendelea kujenga taifa lao pamoja na kuhakikisha wanamtanguliza Mungu kwa kila jambo.

# Jumba la kihistoria laporomoka Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JUMBA la kihistoria Zanzibar, maarufu Jumba la Maajabu (Beit-ajabu), limeporomoka wakati mafundi wakiendelea kulifanyia matengenezo.

Hadi tunaingia mtamboni jana, watu wanne walikuwa wameokolewa na kukimbizwa hospitalini baada ya kufukiwa na kifusi. Jengo hilo ambalo lilijengwa mwaka 1883 na Mfalme Sultan Barghash Said na Serikali ya Zanzibar inalitegemea kimapato kutokana na watu mbalimbali wakiwamo watalii kutembelea na kufanya utafiti. Jengo hilo liliporomoka jana majira ya saa sita mchana wakati mafundi wakiwa katika harakati za ujenzi, ambapo baada ya tukio hilo, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alizuru kuona shughuli za uokoaji.

Akiwa katika eneo hilo akiambatana na viongozi mbalimbali wa serikali, Dk. Mwinyi aligiza hatua za haraka za uokoaji zifanyike ili kuwanusuru watu waliofukiwa na kifusi kupatikana wakiwa hai.

"Zoezi la uokoaji linaendelea vizuri, Mungu asaidie liendelee vizuri, ili kuokoa maisha ya watu ambao wamefukiwa na kifusi," alisema Dk. Mwinyi.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamishna wa Kikosi cha Uokoaji cha Zimamoto, Haji Gora, alisema juhudi za uokoaji zilikuwa zinaendelea na bado sauti za watu zilikuwa zinasikika kutoka kwenye kifusi.

"Tayari watu wanne tumeshawapata wapo hai ambao walifukiwa na kifusi na wameshakimbizwa hospitalini, hivyo tunaendelea kuwatafuta wengine ili kuokoa maisha yao," alisema.

Katika kipindi cha sherehe za Krismasi na Mwaka Mpya, watalii wa nje na ndani hutembelea vivutio vya utalii na hasa jumba hilo, ambalo limeshehеni historia kuhusu Zanzibar na ubunifu mkubwa juu ya usanifu wa majengo kwa kutumia teknolojia ya kipekee.

Kwa mujibu wa Idara ya Mambo ya Kale Zanzibar, jumba hilo huonekana la ajabu kutokana na ujenzi wake na ni la kwanza kutumia nishati ya umeme kwa miaka hiyo na maji ya bomba na lina nguzo zaidi ya 40 zilizojengwa kwa ustadi mkubwa.

# Askari wawili JWTZ wafa ajali ya pikipiki

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

ASKARI wawili wa Jeshi la Wananchi (JWTZ) kutoka vikosi vya Chaburuma Songea Mjini na Mlale JKT mkoani Ruvuma, wamefariki dunia baada ya pikipiki waliyokuwa wakisafiria kugongana na gari la Idara ya Misitu kwenye barabara ya Songea-Njombe katika Kijiji cha Ngadinda wilayani Songea.

Akizungumza na Nipashe jana, kuhusu tukio hilo, Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Pili Mande, alisema tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa 10 jioni. Aliwataja waliofariki dunia kuwa ni Atusubisye Fongo (27), askari wa JWTZ Kikosi cha Chaburuma na Festo Mnimbo (29), askari wa JWTZ Kikosi cha JKT Mlale wilayani Songea.

Alisema kuwa siku hiyo ya tukio, gari lenye namba za usajili STK 1819 aina ya Nissan Patrol, mali ya Idara ya Misitu, lililokuwa likiendeshwa na John Ponela (43), likitoka Songea Mjini kwenda Kijiji cha Wino, liligongana na pikipiki aina ya Hunter iliyokuwa ikiendeshwa na Fongo aliyekuwa amembeba Mnimbo na kusababisha vifo vyao papo hapo.

Mande alisema chanzo cha ajali hiyo ni mwendokasi wa madereva wote wawili.

Alisema kuwa dereva wa gari, Ponela, anashikiliwa na Jeshi la Polisi na upelelezi wa tukio hilo ukikamilika, atafikishwa mahakamani.

# Lissu: CHADEMA msikate tamaa

**Na Enock Charles**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, ametuma salamu za Krismasi kwa Watanzania, akiwataka wanachama na wafuasi wa chama hicho kutokata tamaa katika jitihada zao alizoziita mapambano ya kudai haki. Vilevile, mtaalamu huyo wa sheria, ameahidi kuwa Januari Mosi, atatoa mwelekeo wa chama hicho na mikakati mbalimbali kwa mwaka ujao.

Lissu ambaye amekuwa kimya tangu kumalizika kwa Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu, kwa sasa yuko Ubelgiji alikokwenda kutokana na kile alichodai sababu za usalama wake akihofu kuwapo watu wanaomfuatilia kwa malengo mabaya.

"Kwa wote hawa wenye njaa na kiu ya haki, ujumbe wangu wa Krismasi ni uleule alioueleza mwandishi wa riwaya wa Kimarekani, Taylor Caldwell: "Hatuko peke yetu. Hata usiku unapokuwa wa giza zaidi, au upepo wa baridi kali, au ulimwengu unapoonekana kutokujali kabisa.

"Hatuko peke yetu. Kwa hiyo tusivunjike moyo au kukata tamaa. Wiki ijayo, katika salamu zangu za Mwaka Mpya, nitazungumza kwa kirefu kidogo juu ya masuala haya na mengine na juu ya majukumu yetu kwa mwaka ujao," alisema Lissu katika kipande cha video.

Lissu alishika nafasi ya pili katika Uchaguzi Mkuu uliopita nyuma ya Rais John Magufuli.

Kabla ya kuanza kwa kampeni za uchaguzi huo, mbunge huyo wa zamani wa Singida Mashariki, alikuwa anaishi Ubelgji alikokwenda kwa ajili ya matibabu ya kibingwa baada ya kushambuliwa kwa risasi jijini Dodoma na watu wasiojulikana miaka mitatu iliyopita.

HABARI KITAIFA

# Aweso aipa siku 14 DAWASA kumaliza tatizo la maji Dar

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, ametoa siku 14 kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kuhakikisha wakazi wa Mtaa wa Golani, eneo la Mnazimmoja, Kata ya Kimara wilayani Ubungo, wanapata huduma ya majisafi.

Alitoa agizo hilo juzi, alipowatembelea wakazi wa mtaa huo, kwa lengo la kutatua kero ya ukosefu wa maji waliyonayo kwa muda mrefu. Waziri huyo alifuatana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Uwekezaji, Profesa Kitila Mkumbo, ambaye ni Mbunge wa Ubungo.

"Kwa kuwa mna miundombinu na uwezo mnao, mnaweza kukamilisha kazi hii ndani ya siku 14 kuanzia leo (juzi). "DAWASA mnafanya kazi nzuri sana, ninataka kuona wananchi wa Mtaa wa Golani wanapata maji ndani ya siku 14.

"Kwa kuwa mmeweza kufikisha maji kwenye maeneo mengine ndani ya jiji ikiwamo Kifuru kwa gharama kubwa, ninajua hamtashindwa kufikisha maji kwenye Mtaa wa Golani kwa muda huo," Aweso aliagiza.

Akiwahakikishia huduma wakazi wa Golani, Ofisa Mtendaji Mkuu wa mamlaka hiyo, Cyprian Luhemeja, alisema tayari mabomba ya kusambaza maji kwenye eneo la kilomita 3.7 yameshafika eneo la mradi.

"Kutokana na eneo hili la Mnazimmoja kuwa na milima, tumesanifu mtandao wa maji ambao hautaguswa na mtandao mwingine, na mpaka sasa tumeshasanifu mradi kwa ajili ya kupitisha mabomba ya maji kwenye eneo la mtandao wenye urefu wa kilomita 3.7.

"Hivyo, mradi utahusisha ulazaji bomba kwenye mtandao kwa kuanza na inchi 12, baadaye itakuja inchi 10, baadaye inchi nane na mpaka hapa Golani itafika inchi sita. "Kazi imeanza leo na tutaikamilisha baada ya siku 14 kwa kushirikiana na wananchi," aliahidi.

Mradi wa maji Golani unatarajiwa kunufaisha zaidi ya wakazi 1,000 wa mtaa wa huo ambao wamekuwa kwenye adha ya kukosa maji kwa muda mrefu. Kuhusu kero ya maji maeneo ya pembezoni mwa Jiji la Dar es Salaam, Ofisa Mtendaji Mkuu, amesema tayari DAWASA imepata ufadhili kutoka Benki ya Dunia (WB) Sh. bilioni 115.

Alisema kuwa kwa kazi ya Kibamba jijini, wametenga Sh. bilioni 67 na kazi imeshaanza na wamelaza kilomita 180 Mabwepande na kilomita 86 Bagamoyo.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Uwekezaji), Profesa Mkumbo, aliwataka wananchi wa Golani kuhakikisha wanashirikiana na serikali kupitia DAWASA kulinda na kutunza mradi wa maji ili uwe na manufaa kwa wote.



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul (kushoto), akiteta jambo na Mbunge wa Longido, Dk. Stephen Kiruswa (kulia), walipokutana katika mkutano wa wafugaji na Naibu Waziri huyo, uliofanyika katika eneo la mnada wa mifugo, lililopo Kijiji cha Orendeke, Namanga Mpakani, wilayani Longido, mkoani Arusha juzi. Katikati ni Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Prof. Elisante Ole Gabriel. **PICHA: MBARAKA KAMBONA**

# Watoto saba wajeruhiwa kwa kuangukiwa na nyumba

**Na Jumbe Ismailly,** IGUNGA

WATOTO saba wa Mtaa wa Stoo, Kata ya Igunga Mjini, akiwamo mmoja mwenye umri wa wiki tatu, wamenusurika kufa na wengine wawili kujeruhiwa vibaya kutokana na kufuatia mvua kubwa inayoendelea kunyesha.

Mvua hiyo iliyoambatana na upepo mkali imesababisha nyumba za kaya 18 kuezuliwa na upepo na zingine kuanguka na kuwaponda watoto hao.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Stoo, Fabiani Lushindika, alibainisha kuwa tukio hilo lilitokea Desemba 23, mwaka huu, saa 10:30 nusu jioni kutokana na mvua kubwa iliyonyesha kwa takribani dakika 25.

Alisema nyumba hizo zilianguka na watoto hao kukandamizwa na kuta za nyumba hizo na kwamba watoto wawili walijeruhiwa vibaya kwenye maeneo ya kichwani na usoni.

Lushindika alisema baada ya mvua hiyo kukatika, walifukua vifusi vya nyumba hizo na kuwatoa watoto hao na kisha kuwapeleka katika Hospitali ya Wilaya kwa ajili ya kupatiwa matibabu na hadi jana walikuwa wamelazwa hospitalini hapo.

Alisema kutokana na mvua hiyo, kaya 18 zenye familia za watu 58, hazina mahali pa kuishi, hivyo kumuomba Mbunge wa Igunga, Nicolaus Ngassa, kuangalia uwezekano wa kuzisaidia makazi ya muda.

Ngalu Masele, ambaye mtoto wake Masele Ngalu (12 ) alijeruhiwa usoni na kichwani ambaye amelazwa hospitalini hapo, alisema wakati upepo ukiezuwa mabati ya nyumba yake, mtoto wake alikuwa ndani na yeye alikuwa nje ya nyumba hiyo.

Alisema wakati mvua hiyo ikinyesha, aliona ukuta wa nyumba ukianguka na kumponda mwanawe na kwa kusaidiana na majirani, walitoa kifusi na kufanikiwa kumwokoa.

Mzazi huyo aliwashukuru wauguzi na madaktari waliokuwa zamu kwa juhudi walizozifanya za kuokoa maisha ya watoto hao saba kwa kuwa waliweka mbele maslahi ya majeruhi bila kutanguliza kwanza gharama za matibabu.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Igunga, Merchades Magongo, alikiri kuwapokea watoto hao huku baadhi yao wakiwa wamejeruhiwa vibaya katika sehemu mbalimbali za miili.

Aliwataja watoto hao kuwa ni Eva Peter ( 3), Zainabu Juma (2), Masele Ngalu (12), Amina Ismail (2), Baraka Augustino (11), Daniel Samuel wa umri wa wiki tatu na Yunus Daniel (12).

Alisema Amina Ismail na Zainabu Juma hali zao si nzuri kutokana na majeraha waliyopata kwenye maeneo ya kichwani, usoni na mkononi.

Mbunge Ngasa licha ya kutembelea, kukagua na kuzungumza na baadhi ya wananchi wa mtaa wa Stoo, alitoa msaada wa fedha kwa baadhi ya familia kwa ajili ya kununulia chakula.

Pia alisema ameshawasiliana na Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Igunga, ili watoto hao wapatiwe matibabu bure na alishaandaa mazingira kitengo cha maafa ili familia hizo zisaidiwe kwa muda mahali pa kuishi.

# Waziri aamuru kukamatwa kwa watuhumiwa utoroshaji madini

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

WAZIRI wa Madini, Doto Biteko, ameamuru kukamatwa kwa watu 11 wanaonunua madini nje ya mfumo na kuyatorosha na kubainisha kuwa watu hao wana mtandao wa watu wanaoingia Kahama kununua madini hayo kinyume cha utaratibu.

Biteko alibainisha hayo juzi, alipofanya ziara ya kushtukiza katika machimbo ya dhahabu ya Mwime, wilayani Kahama hapa kwa lengo la kukutana na wachimbaji wadogo.

"Mnaweza kuamini kuwa kwenye soko lenu kwa siku, dhahabu inayoingia kwenye mfumo wa serikali ni gramu 167. Kwa hiyo tumekamata hao manyangumi wenu na baada ya kuwakamata jana (juzi) saa sita mpaka jioni gramu zilizopatikana ni zaidi ya 600," alisema.

"Kuna wizi mkubwa wa dhahabu unaotokana na utoroshwaji uliokithili. Leo (juzi) asubuhi tumechukua watu wawili kuanzia asubuhi hadi saa saba wameshanunua gramu 700, maana yake mpaka kufika jioni dhahabu itakayokuwa imenunuliwa itakuwa zaidi ya kilo moja na tumekamata watu wachache tu," aliongeza.

Pia Biteko aliwaambia wananchi hao kuwa mpaka sasa dhahabu ya mercury inapatikana kwenye soko la dhahabu Kahama na kuongeza kuwa dhahabu hiyo, ilikuwa haionekani badala yake iliyokuwa ikionekana ni ya kwenye 'elution plant' huku akisema kuwa hiyo ya mercury wanauziana kinyemela.

"Nataka niwaambieni hamtafanikiwa. Yeyote anayedhani anaweza kucheza hatafanikiwa na hao tuliowakamata lazima nianze na mtu wangu. Pale kuna ofisa anayesimamia soko, kwenye regista yake tumejumlisha tukakuta ana gramu 600 kwa wote, lakini sisi tumechukua wawili tumejumlisha na kupata zaidi ya gramu 700," alisema Biteko.

Alisema anategemea maofisa madini wamsaidie, lakini kutokana na wizi huo alimwelekeza Mtendaji wa Tume ya Madini amsimamishe kazi mara moja Ofisa Madini, Isaya Rock.

Biteko pia alitangaza kumsimamisha kazi Mwenyekiti wa Soko la Madini la Mwime, Samweli Malimi na kutotakiwa kufanya shughuli zozote katika soko hilo.

Sambamba na hilo, Waziri Biteko aliielekeza Tume ya Madini kusimamisha leseni zilizohusika kwenye udanganyifu, ili uchunguzi ufanyike na hatua ichukuliwe kwa wahusika ikiwa ni pamoja na kuwafutia leseni na hawatoruhusiwa tena kufanya biashara ya madini.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wachezaji, viongozi Ligi Kuu simamieni nidhamu

**WAKATI** mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara umeshamalizika kwa baadhi ya timu zinazoshiriki ligi hiyo, bado suala la nidhamu limekuwa ni tatizo kwa wachezaji, makocha na viongozi.

Timu ambazo hazijakamilisha idadi ya mechi 17, ni zile ambazo zinakabiliwa na michezo dhidi ya wawakilishi wa nchi wanaopeperusha bendera ya Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa yanayoendelea chini ya usimamizi wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Wawakilishi hao ni Simba ya jijini Dar es Salaam inayoshiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika pamoja na Namungo FC ya mkoani Lindi, ambao wanashiriki Kombe la Shirikisho Afrika, ikiwa ni mara ya kwanza kucheza michuano hiyo.

Kutokana na kalenda hiyo ya kimataifa, Simba, Namungo na baadhi ya timu zimecheza mechi chache, hivyo utakapoanza mzunguko wa pili, watakuwa na viporo watakavyolazimika kuvicheza huko mbele.

Hata hivyo, wakati ligi hiyo inaendelea, Nipashe imeshuhudia nidhamu ndogo inayoonyeshwa na wachezaji, viongozi, makocha, mashabiki na wanachama wa klabu mbalimbali hapa nchini.

Kumekuwa na tabia ya wachezaji kufanya makosa yanayojirudia ambayo hayapendezi kuonekana kwenye ligi hiyo ambayo inaonyeshwa mubashara na hivyo, matukio hayo kuonekana sehemu mbalimbali duniani na kuitia nchi doa.

Gazeti hili linawakumbusha wachezaji, viongozi na makocha kuwa mfano wa kuigwa kwa kubadilika wakati mzunguko wa pili utakapoanza na kuziepusha klabu zao na faini za mara kwa mara kwa matukio ambayo yanazuilika.

Ni aibu katika dunia hii ya utandawazi kwa klabu za Ligi Kuu Tanzania Bara kuamua kuingia viwanjani kwa kuruka ukuta au kutumia milango inayotumiwa na mashabiki kwa kile kinachoaminika kukwepa 'ushirikina'.

Tunawakumbusha timu itakayopata matokeo mazuri ni ile ambayo itaonyesha kiwango bora, itakayowekeza nguvu zake kwenye maandalizi sahihi na kamwe si ile inayoamini nguvu za giza au miujiza.

Haipendezi kuona timu ya Ligi Kuu Tanzania Bara inaadhibiwa kwa matukio ambayo yanachangia kushusha heshima ya timu husika hata kama viongozi wake watakuwa tayari kulipa faini watakayoadhibiwa, kwa sababu kwa kufanya hivyo hakujengi na kunarudisha nyuma maendeleo ya soka.

Nidhamu mbaya au ya kiwango cha chini inachangia kuwaharibu wachezaji chipukizi ambao wamekuwa wakishuhudia matukio mbalimbali yanayoendelea kwenye televisheni na hivyo kubakia kwenye akili zao.

Ushauri huu wa kusimamia nidhamu unawahusu pia wachezaji, viongozi, makocha na mashabiki ambao timu zao pendwa zinashiriki Ligi Daraja la Kwanza au Ligi Daraja la Pili, kwa sababu klabu hizo zina nafasi ya kupata tiketi ya kucheza mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika endapo watatwaa ubingwa wa Kombe la FA Tanzania.

Ni aibu na ni jambo linaloonekana kiongozi kutojua kanuni kwa kusikika hadharani akitoa shutuma dhidi ya timu pinzani, waamuzi au kwa shirikisho, hali ya kuwa njia stahiki za kuwasilisha malalamiko yao wanazifahamu.

Hatutegemei kuona makosa ya kinidhamu yaliyofanywa wakati wa mzunguko wa kwanza yanajirudia tena kwenye hatua ya lala salama na badala yake tunawakumbusha viongozi kufanya majukumu yenu kwa weledi.

Ikumbuke Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya Kombe la FA, ndio hutoa wawakilishi wa nchi kwenye mashindano ya kimataifa yanayofanyika kila mwaka, hivyo ni bora kuwaandaa wachezaji na viongozi wenye nidhamu ambao watazisaidia klabu zao kuwekeza nguvu katika kusaka ushindi tu.

Tunaamini ili kuwa na kizazi wanasoka walioandaliwa vyema kusakata kandanda kwa kiwango cha juu, ni wakati wa wadau wote wanaohusika kuhakikisha wanasimamia nidhamu na wanaionyesha kwa vitendo wanapokuwa ndani na nje ya uwanja.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Barnabas Maro

## Muungwana Lazima Nilonge

# Ni dhahiri TFF imeshindwa ...!

**"DHAHIRI"** maana yake ni -liowazi, bila kificho, bayana, jahara. Ndivyo Shirikisho la Soka Nchini linavyoendelea kutimiza wajibu wake ipasavyo?

"Sheria" ni taratibu maalumu zenye vifungu mbalimbali zinazotungwa na chombo chenye mamlaka kusimamia taratibu za utekelezaji wa jambo.

Kwa hiyo TFF ina wajibu wa kusimamia kanuni zinazoelekeza jinsi mchezo husika, hasa kandanda inavyopaswa kusimamiwa na kuendeshwa kwa sheria na haki.

Kuhakikisha timu zinafuata taratibu zote za mchezo kama vile idadi ya wachezaji wanaotakiwa uwanjani, wachezaji wa akiba, taratibu zinazotawala mchezo husika na adhabu inayostahili pindi kosa linapofanywa na wachezaji au wasimamizi.

Kwa hiyo mwamuzi apaswa kuzingatia sheria 17 za mpira wa miguu awapo uwanjani. Je, waamuzi wa Tanzania wanafuata sheria za mpira wa miguu au wanatawaliwa na 'U-Simba na 'U-Yanga'?

Kama si 'U-Simba' na 'U-Yanga,' basi ni kile walichosema wahenga: "Fedha fedheha." Kwamba pesa huweza kuleta mambo ya aibu baina ya binadamu. Ndivyo ilivyo sasa!

Twaonywa kuhusu maovu yanayoweza kusababishwa na pesa. Ndio sababu ilisemwa: "Fedha ilivunja nguu milima ikalala." Maana yake pesa zina uwezo wa kuivunja milima na vilima!

Je, Simba na Yanga hutumia fedha ili zipate ushindi hata kama wachezaji wao wanafanya kinyume cha sheria na taratibu za mchezo wa kabumbu? Tafakari.

"Haki" ni jambo linalomstahikia mtu; utendaji, ufuataji na utumiaji wa sheria na kanuni katika kutimiza jambo.

Twakumbushwa kwamba aghalabu/aghlabu (hali ya kutokea jambo mara nyingi) mtu mwenye tabia ya kuusema ukweli huaminiwa na watu wengine. Ni vizuri tuwe na tabia ya kusema kweli ndipo tuaminiwe.

"Kusema kweli si tua." Maana ya 'tua' ni aibu au fedheha. Kwa hiyo kusema kweli si kwa kuonewa aibu wala sio ila. Hutumiwa kuwahimiza binadamu kuwa na tabia ya kusema kweli bila woga au kusita.

Je, waamuzi wa kandanda nchini huamua kwa haki, bila kuzipendelea timu wazipendazo au ni kile walichosema wahenga kuwa "Kipenda roho hula nyama mbichi?"

Waamuzi wasiofuata sheria na kanuni za kabumbu hupendelea waziwazi na kuzinufaisha timu wazipendazo au zilizowapa chauchau (rushwa) ili zipendelewe!

Kuna wakati huwa na hisia (hali ya kiungo cha mwili kama vile ubongo, ulimi au moyo kutambua jambo) kwamba huenda waamuzi wanaopokea rushwa hufanya hivyo kwa kutolipwa stahiki zao!

Fedha zinazoingizwa na watazamaji, hasa zichezapo Simba na Yanga dhidi ya timu zingine hazitoshi kuwalipa waamuzi? Ni wazi kuwa TFF huwa na kiasi fulani cha fedha za viingilio vya wanaoingia viwanjani.

Kama ndivyo ilivyo, TFF yenye viongozi wengi wanachama au wenye mahaba (mapenzi) kwa Simba na Yanga wanapaswa kuwajibishwa kwani matokeo ya rushwa na upendeleo yanaharibu maendeleo ya kandanda nchini.

"Rushwa" ni fedha au kitu chochote cha thamani apatiwacho mtu mwenye uwezo au madaraka katika jambo fulani ili amfanyie mtoaji hisani au upendeleo.

Kwa maana nyingine yaitwa mrungura/ mlungula, kadhongo, hongo au chai. Kwa hiyo 'rushwa' ni adui wa haki.

Nieleze mifano mitatu ya wazi iliyotokea Mwanza, ambapo timu ya Yanga ilipewa penalti isiyo halali ilipocheza na KMC ya Kinondoni na kuipa Yanga ushindi wa mabao 2-1.

Jijini Dar es Salaam, Simba nayo ilipewa penalti yenye utata mwamuzi akisema eti mchezaji wa KMC aliushika mpira wakati haikuwa hivyo.

Hata marudio ya runinga yalionesha kuwa mwamuzi hakufanya haki kwani mchezaji wa KMC 'hakuunawa' mpira kama alivyoamua mwamuzi! Kwa hiyo mechi ya KMC dhidi ya Yanga ilipaswa kuwa sare ya 1-1 ilhali ile ya KMC na Simba ingekuwa suluhu yaani bila kufungana.

Mchezo baina ya Yanga na Dodoma Jiji uliochezwa Arusha, refa alishangaza kwa jinsi alivyokuwa na ghadhabu kana kwamba alishurutishwa kuchezesha mchezo ule!

Mchezaji wa Yanga aliyechezewa rafu na kumlalamikia mwamuzi, eti mlalamikaji ndiye aliyeadhibiwa kwa kuoneshwa kadi ya njano!

Yeye ndiye aliyeangushwa na mchezaji wa Dodoma Jiji, timu iliyofanya faulo mara 30 dhidi ya 8 zaYanga!

Tugeukie upande mwingine unaohusu ujinga wa baadhi ya mashabiki wa Simba na Yanga wanavyoshangilia mojawapo inaposhindwa na timu ngeni.

# HABARI PICHANI



Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Ushirika wa Sinza (KKKT), Ibrahimu Munanka, akitoa baraka za Krismasi kwa watoto waliofika kwenye ibada hiyo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Wateja wakichagua kuku kwa ajili ya kitoweo cha sikukuu ya Krismasi katika eneo la Kimara Mwisho, jijini Dar es Salaaam jana, kuku mmoja aliuzwa kwa Sh. 25,000. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Waumini wa Kanisa la KKKT la jijini Dar es Salaam, wakifuatilia ibada iliyokuwa ikiongozwa na Askofu Mkuu wa Kanisa hilo, Alex Malasusa, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Waziri Mkuu mstaafu, John Malecela, akisalimiana na Askofu wa Kanisa la Angalikana Dayosisi ya Centre Tanganyika Dodoma, Dk. Dickson Chilongani, baada ya kumalizika kwa misa ya ibada ya sikukuu ya Krismasi iliyofanyika kanisa kuu jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**



Baadhi ya waumini ya dini ya Kikristo Kanisa la Kiinjili la Kiluther Tanzania (KKKT), Usharika wa Dodoma Mjini, wakishiriki ibada ya sikukuu ya Krismasi ambayo ilifanyika jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**



Waumini wa Kanisa la Mtakatifu Alban's, wakiwa kanisani katika Ibada ya sikukuu ya Krismasi, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Shule kwenda kidijitali kushirikiana na za nje

**Na Mwandishi Wetu**

SHULE za St Mary's zimedhamiria kwenda kidigitali kwa kushirikiana na shule za nje ya nchi, ili kuboresha mifumo yake ya kompyuta na kuzifanya kwenda kisasa zaidi.

Ahadi hiyo ilitolewa juzi na mmoja wa wakurugenzi wa shule hizo, Mutta Rwakatare, wakati akizungumza kwenye mahafali ya 22 ya Shule ya Awali St. Mary's Mbagala jijini Dar es Salaam.

Mutta alisema wanaandaa utaratibu, ambapo watakuwa wanabadilishana wanafunzi na walimu wa shule za nje ya nchi ambapo watakuwa wakienda na kurudi kwa ajili ya kuongeza maarifa.

"Huu ni mpango mkakati wa shule zetu zote ikiwa ni kwa ajili ya kuboresha taaluma za shule zote za St. Mary's zilizopo Dar es Salaam, kuanzia hii ya Mbagala, Tabata, Mbezi, Dodoma, Ifakara, Mbeya na Morogoro," alisema.

Mutta alisema wana mpango wa kuboresha madarasa yatakayokuwa yanatoa elimu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na mifumo ya kompyuta kwa wanafunzi.

Alisema lengo la kufanya hivyo ni kuhakikisha watoto kuanzia darasa la kwanza mpaka darasa la saba wanapata ujuzi wa kutumia kompyuta kutokana na mabadiliko ya kiteknolojia kwa karne ya sasa.

Katika kufanya hivyo, alisema wataweka mkazo katika michezo ili kuwasaidia wanafunzi ambao watakuwa na vipaji mbalimbali katika michezo kwa kuwapa walimu ambao wanafundisha michezo ile, ili kukuza vipaji vyao.

Aliwaomba watu ambao hawajawapeleka watoto wao katika Shule za St. Marry's kuwapeleka ili wakapate malezi bora na yenye tija kwa jamii kutokana na maboresho makubwa yanaendelea katika shule zote.

"Kuna maboresho makubwa ambayo tunayafanya katika shule zetu, miundombinu, mabweni, madarasa pamoja na mifumo ya kompyuta, ili kuhakikisha watoto wanaishi vizuri wawapo shuleni na kupata elimu iliyo bora," alisema.

Katika mahafali hayo watoto walionyesha vipaji vyao katika kuimba, kuelezea mfumo wa chakula pamoja na kuonyesha mitindo mbalimbali ya mavazi na ustadi katika miondoko ya mitindo hiyo.



Baadhi ya wananchi wa Manispaa ya Songea, Mkoa wa Ruvuma, wakinunua mapambo mbalimbali kwa ajili ya Krismasi kwenye maduka yaliyopo barabara ya Sokoine Kata ya Mjini mkoani humo. **PICHA: MICHAEL EMMANUEL**

# Jaji ataka watu kukumbuka walikotoka

**Na Francis Godwin,** IRINGA

JAJI wa Mahakama Kuu, Paul Ngwembe, amewataka viongozi wa vijiji, kata na Wilaya ya Mufindi mkoani Iringa, kuwaunganisha wasomi kwenye maeneo yao, ili wasaidie maendeleo katika maeneo wanayotoka.

Ngwembe alitoa rai hiyo, juzi, wakati akizindua kitabu alichokiandika kuhusu historia ya Kijiji cha Nyanyembe, Kata ya Mbalamaziwa Wilaya ya Mufindi.

Alisema changamoto kubwa iliyopo kwenye vijiji ni kukosekana kwa umoja wa wasomi hao katika kuleta mabadiliko zaidi ya kijiji chao.

"Hakuna chombo kinachowaunganisha pamoja wasomi, ili walete mchango wao katika ustawi wa vijiji vyao hadi wilaya wanazotoka. Mabadiliko ni lazima yawapo kwani ni ukweli kwamba kubadilika, tubadilishwe na tukikataa tutabadilishwa basi tutasahaulika maana tulitembea gizani sasa tunaona nuru," alisema.

Pia alisema jamii lazima iache mazoea na kutenda kwa ukakamavu mambo ya karne ya 21 na kwamba busara na hekima ni kujua asili.

"Asili itatujuza tuendako na kitabu cha Historia ya Nyanyembe kimesheheni ukweli juu ya asili yako," alisisitiza.

Jaji Ngwembe alimnukuu Rais mstaafu wa Marekani, Barack Obama, aliyewahi kusema: "Mabadiliko hayawezi kutokea iwapo sisi Marekani tutawasubiri wengine wafanye kwa muda mwingine. Sisi ndio wahusika tuliokuwa tunasubiriwa kuleta mabadiliko haya na sisi ndio mabadiliko yenyewe."

Akielezea mchango chanya wa kanisa na serikali, alisema umekifanya kijiji cha Nyanyembe kuwa na wasomi wa vyuo vikuu wapatoa 85 wakiwamo watatu waliojiunga na vyuo vikuu mwaka huu, ambao miongoni mwao wamo wenye shahada za uzamili 18 na wanasheria tisa.

Pia alisema wamo madaktari sita, mhandisi mmoja, walimu wanaofundisha vyuo vya elimu ya juu wanne, walimu wa sekondari wengi, maofisa mipango na maendeleo ya jamii na wahasibu ambao majina yao ameyaweka kwenye kitabu hicho.

Jaji Ngwembe alisema kitabu hicho kimekusanya taarifa zote muhimu tangu kuanzishwa kwa kijiji hicho mwaka 1900 hadi 2019 na kuandika kwa mtiririoko chanya wa kihistoria.

# Mbunge alia malipo wahudumu corona

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MBUNGE wa Viti Maalum Mkoa wa Pwani, Hawa Mchafu, ameiomba serikali kuwalipa watumishi waliokuwa wakihudumu katika kambi ya wagonjwa wa corona, Lulanzi mjini Kibaha.

Mchafu alitoa maombi hayo juzi, mjini hapa, katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa wa Pwani.

Alisema watumishi hao wa afya ambao walikuwa katika kambi hiyo hadi sasa hawajapata malipo yao.

"Wamenifikishia hizi taarifa na nimelazimika kuzifikisha hapa tupate majibu ya kinachoendelea. Nitaenda kuwasemea pia bungeni ili wapate haki yao kwani zaidi ya miezi mitatu imepita tangu kituo kifungwe, lakini hakuna walichopata hadi leo pamoja na kufanya kazi zao usiku na mchana," alisema Mchafu.

Alisema watumishi hao walimweleza kuwa walielezwa kupeleka taarifa za namba za akaunti za benki, lakini hadi sasa hakuna malipo yaliyofanyika na kwamba hawajapewa taarifa kuhusu kinachoendelea.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Dk. Gunini Kamba, alisema taarifa za watumishi hao waliokuwa katika kambi ya wagonjwa wa corona tayari wamezifikisha Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsi, Wazee na Watoto kwa taratibu zaidi.

Kwa mujibu wa Dk. Kamba, watumishi wote waliokuwa katika kambi za corona hakuna aliyepata malipo hadi sasa kwa nchi nzima, hivyo tatizo hilo si la mkoa wa Pwani pekee.

HABARI KITAIFA

# Wizara yawapa somo wamiliki wa hoteli upangaji madaraja

**Na Ibrahim Joseph,**
DODOMA

KATIBU Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Aloyce Nzuki, amewataka wamiliki wa hoteli na nyumba za kulala wageni, kujisajili kwenye mfumo wa kielektroniki ili kuwapanga katika madaraja ya ubora.

Dk. Nzuki alitoa kauli hiyo juzi, wakati alipozungumza kwenye uzinduzi wa mfumo wa upangaji huduma za malazi katika madaraja ya ubora kwa njia ya kielektroniki uliofanyika jijini hapa.

Aliwataka wamiliki wa hoteli zote pamoja na nyumba za malazi, kuhakikisha wanajisajili kwenye mfumo huo, ili kurahisisha kuwapanga katika madaraja ya ubora.

"Mfumo huu utawezesha wamiliki wa huduma za malazi na hoteli kufanya tathmini binafsi ya huduma wanazozitoa kwa mujibu wa vigezo na kupanga madaraja ya ubora wa nyota wao wenyewe kabla ya kuthibitishwa na wathamini wa serikali," alisema.

Mtendaji huyo wa wizara pia alisema serikali imezindua mfumo wa kielektroniki wa tathmini ya upangaji huduma za malazi na chakula katika ubora wa madaraja ili kupunguza gharama na muda wa kufanya uhakiki uliokuwa ukitumika siku za nyuma.

Aliutaja mfumo huo kuwa unajulikana kwa jina la Accommodation Services in Tanzania (Asert) na unalenga kurahisisha tathmini ya upangaji wa huduma hizo katika ubora wa madaraja au nyota.

Alisema mfumo huo ni maboresho ya mfumo uliokuwapo, akidokeza kuwa wa sasa umezingatia vigezo vyote vinavyotumiwa na nchi za Afrika Mashariki na kimataifa.

Dk. Nzuki alisema mfumo huo utapunguza malalamiko ya wadau kuhusu ugawaji wa viwango vya ubora wa nyota kwa sababu wadau watajipima wenyewe kabla ya timu ya watu kutoka serikalini kutoa daraja. "Kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wamiliki na wadau wengine kuwapo kwa tuhuma za rushwa, hivyo mfumo huu unakwenda kumaliza kabisa malalamiko hayo na kufanya sekta ya malazi nchini kuwa ya ushindani zaidi," alisema.

Kaimu Mkurugenzi Idara ya Utalii, Philip Chitaunga, alisema huduma za malazi nchini zilizopangwa kwa ubora, zimeongezeka kutoka 67 mwaka 2015 hadi kufikia 308 kwa mwaka 2020.

Alisema kazi ya upangaji huduma za malazi katika ubora imeshafanyika katika mikoa mitano ambayo ni Dar es Salaam, Pwani, Manyara, Arusha na Dodoma.

Chitaunga alisema kazi ya kupanga huduma za malazi katika madaraja ya ubora huanzia nyota moja hadi tano na nyota hizo hutolewa kwa kutumia vigezo vilivyowekwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Alisema vigezo vinavyotazamwa katika hoteli vipo zaidi ya 120 kulingana na vigezo hivyo kiwango cha juu cha ubora hupewa daraja la nyota tano na kiwango cha chini hupewa nyota moja, huku zile ambazo hazijapewa nyota hutambulika kama huduma za malazi zilizothibitishwa.

Balozi wa Rwanda nchini, Meja Jenerali Charles Karamba, alisema mfumo huo utasaidia wageni wa kimataifa wanapofika kwenye eneo la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Alisema kuna faida kwa wamiliki wa hoteli na nyumba za kulala wageni zikijulikana kwa ubora kwa sababu watapokea fedha kutokana na aina ya nyota au ubora wa huduma ya hoteli na malazi anayotoa.



Aliyewahi kuwa Waziri wa Maji ambaye ni Mzee wa Kanisa Usharika wa Dodoma Mjini, Mhandisi Gerson Lwenge, akishiriki ibada ya Krismasi pamoja na waumini wanzake jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Askofu ataka vyama vya siasa visake mwafaka

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

ASKOFU wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Kati, Dk. Dikson Chilongani, ameshauri vyama vya siasa nchini vimalize tofauti zao kwa kukaa meza moja na kuzungumza ili kufikia mwafaka wa kupata amani.

Kiongozi huyo wa kanisa alitoa rai hiyo jana alipohubiri katika ibada ya Krismasi katika Kanisa Kuu la Roho Mtakatifu Anglikana jijini Dodoma.

Alisema Tanzania ni nchi ya amani na amani hiyo imejengwa na waasisi waliotangulia, hivyo inatakiwa kulindwa ili nchi iendelee kuonekana kisiwa cha amani.

"Amani inaweza kuonekana kama jambo dogo kwa kuwa hakuna vita, na vita inaweza isiwapo, lakini watu wakawa hawana amani kutokana na kutokuwa na nyuso za furaha kwa yale wanayokutana nayo," alisema. "Hatuwezi kutafuta amani kwa mapambano au mabavu na wakati mwingine tumeona viongozi wa kisiasa wakijitamba kutafuta amani kwa kutumia mabavu au kwa njia ya mabavu, jambo ambalo haliwezi kusaidia kama hawatatafuta amani kwa njia sahihi ya kumtanguliza Mungu na kukaa meza moja," alionya.

Askofu Chilongani pia alisema ili kutunza amani ya nchi, ni lazima kujiepusha na tabia ya kulipiza visasi na kuwa na roho ya kutokuwa na makubaliano.

"Tuzungumze amani, pale panapooneka hakuna amani, kaeni meza moja ili kuweza kujadili changamoto mbalimbali ambazo zipo ili ziweze kutatuliwa kwa mazungumzo.

"Ikumbukwe kuwa hata ndani ya vyama vya siasa, haiwezekani kupatikana amani kama viongozi wa kisiasa hawataweza kukaa meza moja kwani hakuna amani ambayo inaweza kupatikana kwa ubabe au mtutu wa bunduki.

"Jambo lingine muhimu ni kuhakikisha tunakuwa watendaji wa amani sambamba na kujiepusha katika kulipiza visasi," alisema.

Naibu Katibu Mkuu wa Kanisa la Pentecostal Holiness Association Mission Tanzania, Askofu Julias Bundala, amewataka Watanzania kutokutumia siku ya Krismasi kama sehemu ya matumizi mabaya ambayo yatasababisha watoto kushindwa kwenda shule.

Alisema wazazi wanatakiwa kuhakikisha wanaandalia mazingira mazuri watoto ambao wanatakiwa kwenda shule kwa kuwapatia vifaa vyote muhimu ambavyo vinatakiwa.

"Wapo baadhi ya wazazi ambao wataitumia vibaya sikukuu ya leo kwa kufanya matumizi mabaya na kujikuta wanamaliza fedha zote na kushindwa kuwaandalia watoto mazingira mazuri ya kwenda shuleni.

"Msiitumie sikukuu hii vibaya na badala yake mbane matumizi kwa ajili ya maandalizi ya kuwapeleka watoto wenu shule wawe na manufaa kwa baadaye," alishauri.

# Mtafiti awapa siri wafugaji

**Na Renatha Msungu,** KONGWA

TAASISI ya Utafiti wa Mifugo (TALIRI) Kituo cha Kongwa, imewashauri wafugaji kupanda majani ya malisho aina ya Cenchrus Ciliaris ambayo yana uwezo wa kustahimili ukame, ili kuwasaidia katika kipindi cha kiangazi.

Ushauri huo ulitolewa na Mtafiti, Dk. George Fupi wa TALIRI Kongwa katika ziara ya waandishi wa habari iliyoandaliwa na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) kwa wadau hao na watafiti wa Mkoa wa Dodoma na Singida.

Dk. Fupi alisema wafugaji wanapaswa kupanda aina hiyo ya majani kwa sababu yamefanyiwa utafiti na kugundua yanastahimili ukame na hivyo kuifanya mifugo kuendelea kupata virutubisho katika kipindi cha kiangazi.

"Tunawashauri wafugaji kuandaa aina hii ya malisho ya majani kwa sababu yana uwezo sana kustahimili ukame.

"Hata kipindi cha kiangazi, wafugaji wakipanda majani haya hawatakuwa na shida ya kupata malisho ya mifugo," alisema.

Dk. Fupi alifafanua zaidi kuwa aina hiyo ya mbegu ina uwezo wa kutoa tani nne mpaka tisa za majani kwa ekari moja, hivyo wafugaji wakinunua mbegu hizo na kuzipanda katika maeneo yao, watakuwa na suluhisho la uhaba wa majani kipindi cha kiangazi.

Alisema wafugaji wakifanya hivyo watakuwa wamesaidia kuepusha migogoro baina ya wafugaji na wakulima ambayo hutokea pindi mifugo inapovamia mashamba ya wakulima.

Ukiacha mbegu hiyo aina Cenchrus Cirrialis, Dk. Fupi alizitaja mbegu nyingine za malisho zilizofanyiwa utafiti katika kituo hicho kuwa ni Bathriochloa Inschpta, Eragrostis Superba, Paniciam Maximum na Rhodes grass.

Dk. Fupi pia alifafanua kuwa wafugaji wanapaswa kuendana na wakati kwa kufuga kisasa, ili kuondokana na ufugaji holela wa kuhama kutoka sehemu moja na kwenda nyingine, jambo ambalo husababisha uharibifu mkubwa wa mazingira katika maeneo mbalimbali.

Alisema kuwa ili kuondokana na migongano hiyo, wafugaji pia wanapaswa kuzingatia kupanda malisho ya mifugo yao kulingana na hali ya hewa ya sehemu husika.

# Watakiwa kutumia mikopo kikamilifu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

VIJANA wajasiriamali wametakiwa kuzitumia fursa za mikopo zilizowekwa na taasisi za kifedha na mifuko mbalimbali ya hifadhi na uwezeshaji ili kufikia malengo wanayotarajia.

Hayo yalisemwa juzi na Ofisa Mikopo wa Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Safia Mwinyi Abuo, katika mafunzo ya kuwajengea uwezo wajasiriamali yaliyofanyika katika ukumbi wa Walimu Dunga, Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema azima ya serikali ni kuhakikisha wajasiriamali wanawezeshwa ili kuipunguzia serikali mzigo wa vijana wengi kusubiri ajira kutoka serikalini.

Pia alisema mfuko huo wa uwezeshaji umeandaa mikopo kwa ajili ya wajasiriamali, ili kufanikisha matarajio yao, huku akisema mfuko umeshatoa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 4.5 ambazo asilimia 76 ni kwa vijana.

Naye Rajab Ali Machano, Mkuu wa Mfuko wa Uchangiaji wa Hiari wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), alisema mfuko huo ulianzishwa kwa lengo la kuwakomboa wananchi ambao hawamo katika sekta rasmi hasa wajasiriamali ili kuwasaidia wanapopata matatizo.

Kwa upande wake, Ali Shaibu Mussa kutoka Benki ya NMB, alisema wameshatoa mafunzo ya ujasiriamali kwa vijiji 75 na kwamba huwapatia mikopo wajasiriamali hao ili kufikia malengo ya serikali.

Aidha, aliwataka vijana kuachana na dhana potofu za kusema hakuna fursa huku akiwataka vijana kukaa pamoja na kubuni njia zitakazowasaidia kujikwamua na umaskini.

Mafunzo hayo yaliandaliwa na jumuiya ya habari dhidi ya matumizi mabaya ya dawa za kulevya Zanzibar (ZAIADA), ambapo taasisi mbalimbali za fedha na mifuko ya hifadhi na uwezeshaji wananchi kiuchumi zilifungua milango ya fursa kwa wajasiriamali hao.



Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Zanzibar, Agostino Shao, akisali kwenye pango la mtoto Yesu baada ya misa ya sikukuu ya Krismasi iliyofanyika kwenye Kanisa la Mtakatifu Joseph visiwani humo, jana. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Uwekezaji mradi wa maua kufanyiwa mapitio

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amemwagiza Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja kufanya mapitio ya mradi wa maua uliwekezwa ndani ya Kijiji cha Kibumbwi.

Ametaka kazi hiyo ifanyike ndani ya mwezi mmoja na ripoti yake kuwasilishwa katika ngazi ya juu kwa hatua zitakazofuata.

Hemed aliyasema hayo jana alipotembelea kijiji cha Kibumbwi, Kaskazini Unguja kujionea hali halisi ya mazingira ya kijiji hicho pamoja na kujua changamoto mbalimbali zinazowakabili wananchi. Alisema malalamiko ya wananchi waliobahatika kufanya kazi ndani ya mradi huo, bila tija wala kipato yamethibitisha kwamba uwekezaji wa mradi huo wenye miaka 15 sasa hauna mafanikio yoyote kwa wananchi wa eneo hilo.

Kwa mujibu wa Makamu wa Rais, jambo hilo ni kinyume cha malengo ya serikali ya kukaribisha wawekezaji kwa faida ya jamii.

Hemed alisema mwekezaji huyo anatakiwa kuhakikisha anafanya kazi kwa kuheshimu maslahi ya wananchi na endapo atashindwa, serikali ina haki ya kumwondoa na kukaribisha mwekezaji mwengine.

Aliwataka wananchi wa kijiji hicho kutoa ushirikiano kutokana na ahadi zilizotolewa na wakuu alioambatana nao ambao wanasimamia miradi ya kijamii kama barabara, umeme, maji safi na elimu ambayo imekuwa changamoto kupatikana katika kijiji chao.

Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Mohamed Mahmoud, alisema mwanzoni wa mwaka ujao wanategemea wanafunzi wa kijiji hicho kuanza kusoma katika shule iliyojengwa katika eneo hilo.

Alisema hatua hiyo ya dharura ni jambo la msingi ambalo litawasaidia wanafunzi kupunguza changamoto ya kufuata huduma ya elimu masafa ya mbali na kuwaepusha na vitendo vya udhalilishaji vilivyoibuka katika jamii dhidi ya watoto.

Mkuu huyo wa Mkoa alimhakikishia Makamu wa Pili wa Rais kuwa watayafanyia kazi maelekezo aliyoyatoa kwa muda, ili kuhakikisha wananchi wa kijiji hicho wanaondokana na changamoto zote zinazowakabili.

Nao baadhi ya wananchi wa kijiji hicho, walitaja changamoto zinazowakabili kuwa ni ukosefu wa maji, umeme, kituo cha afya na shule.

# Mwinyi awakumbuka yatima Krismasi, Mwaka Mpya

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, ametoa msaada wa vyakula mbalimbali kwa watoto yatima wanaoishi Kijiji cha Kulelea Watoto (SOS) Mombasa na Nyumba ya Kulelea Watoto Yatima Mazizini, Mjini Unguja, kwa ajili ya kusherehekea Sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya.

Akikabidhi vyakula hivyo jana, kwa niaba ya Rais, Mkurugenzi wa Huduma za Rais, Ameir Ali Khatib, alisema msaada huo utawasaidia kwa ajili ya sikukuu na kufarijika kama watoto wenzao.

Katika chakula hicho, alisema Rais alipenda kuwa nao pamoja, lakini kutokana na kutingwa na kazi za kiserikali hatakuwapo na kusema kwa ishara hiyo yuko pamoja nao.

Hata hivyo, aliahidi msaada huo hautakuwa wa mwisho na kuendelea kuwapelekea pale inapohitajika kupatiwa vituo hivyo.

Wakipokea msaada huo, wasimamizi wa watoto hao, walimshukuru Dk. Mwinyi kwa msaada huo na kuahidi kutumia kama ulivyokusudiwa kwa manufaa ya watoto.

Naye Naibu Katibu Mkuu Ustawi wa Jamii, Mwanajuma Majid Abdallah, alitoa shukrani kwa niaba ya serikali na kumshukuru Dk. Mwinyi kwa mwanzo mzuri wa kutoa chakula na mahitaji kwa watoto hao.

Alisema kwa hatua hiyo, Rais ameonyesha kuwajali na kuwathamini ambapo watoto hao wamefarijika na msaada huo.

Katika hatua nyingine, Jeshi la Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi, limeweka mpango kazi madhubuti, ili kuhakikisha wahalifu hawapati nafasi katika kipindi chote cha sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi, Awadh Juma Haji, aliyasema hayo wakati akitoa taarifa kwa vyombo vya habari ofisini kwake Mjini Unguja.

Alisema wako wahalifu wanaotumia siku hizo katika kufanya uhalifu ikiwamo kupora mali zao wananchi hivyo jeshi litafanya doria maeneo yote, ili wananchi kusherehekea sikukuu katika hali ya usalama.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

BT
BURUDANI TELE



MR EAZI YAMEMKUTA HUKO GHANA Ukurasa 14





# MASTAA Wanavyomlilia Godfrey Mngereza

TASNIA ya sanaa na burudani bado inaendelea kukumbwa na jinamizi la kupoteza watu wake muhimu, baada ya jana kuondokewa na Katibu Mtendaji wa Baraza la Sanaa Taifa (BASATA), Godfrey Mngereza.

Mngereza alifariki usiku wa Desemba 24, jijini Dodoma katika Hospitali ya General alikuwa amelazwa akipatiwa matibabu.

Baada ya habari hizo kuthibitishwa na Mwenyekiti wa Bodi ya BASATA, baadhi ya mastaa wamejitokeza kutoa rambirambi zao huku wakieleza kushtushwa kwa kifo hicho.

Waliojitokeza kuelezea hisia zao baada ya taarifa ya kifo cha Katibu Mtendaji hiyo ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, ambaye ni Msemaji Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbasi.

"Nimelazwa General hapa Dom ila kila kitu kitaenda sawa kuhusu tamasha napambana, ni meseji ya mwisho niliyoipokea juzi, Jumanne saa tano na dakika 2 usiku kutoka kwa kaka yangu Godfrey Mungereza, Katibu Mtendaji wa BASATA, leo hatunaye tena katika dunia hii ametutoka, tumuombee sana mola ampe pumziko la amani la milele".

Darasa ameandika "Kila nafasi niliyopata na mzee wangu aliwahi kuniambi 'I am a big fun of you', nakuwa huru kuzisikiliza mahali popote....Heshima yako mzee wetu umefanya ulichokifanya pumzika kwa amani."

Zuchu naye ameandika "Mwenyezi Mungu amsamehe ampe kauli thabiti".

Diamond aliandika katika ukurasa wake wa Istagram "Dah nakosa hata cha kuandika, mkuu si juzi tu tulikuwa Arusha ulikuja kutuunga mkono kwenye ziara yetu ya Tumewasha! Umetangulia Dah! Inshallah Mwenyezi Mungu akulaze mahali pema peponi, Amina.

BASI SAWA

## We Kala kumbe ulikufaga miaka 2000

MSANII wa HipHop, Kala Jeremiah, amewashangaza mashabiki wake baada ya kudai kuna wakati anajiona kama sio binadamu wa kawaida kutokana na maono anayona.

Amesema huko nyuma alisema wanasiasa wengi wa vyama pinzani hawatarudi bungeni, jambo ambalo limetokea kwenye uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 28, 2020.

"Miaka ya nyuma vyama vya upinzani vilikuwa vina nguvu sana kwa sababu ya agenda kuu ambazo hata mimi nilikuwa mmoja wanaosapoti, kama ufisadi na ubadhirifu wa mali za umma, ila amekuja Rais ambaye anashughulikia mambo yote hayo."

"Kuna mheshimiwa mmoja wa upinzani nilikaa naye miezi minne kabla ya uchaguzi, nikamwambia mna shughuli kubwa sana na wasishangae kama watarudi wachache, mimi nadhani nina maono na sio binadamu wa kawaida kuna kipindi nahisi nilikufaga sehemu huko kwenye karne ya 15," ameongeza.



## Akudo Impact yaja na 'Puto'



BENDI maarufu nchini ya Akudo Impact, imeibuka na kibao kipya kiitwacho 'Puto' ambacho kinatarajiwa kurekodiwa hivi karibuni.

Kibao hicho ambacho kimeanza kuchengua mashabiki wa bendi hiyo kila inapofanya maonyesho yake, kimetungwa na kiongozi wa bendi hiyo Zagreb Butamu, maarufu kama 'Sura ya Mvuto'.

Mwanamuziki wa bendi hiyo, Maliki Star amesema kuwa bendi hiyo, imejipanga vema kurudisha makali yake ya zamani kama ilivyokuwa enzi za kina Christian Bella.



## Shamsa acha maneno!

MWIGIZAJI mkongwe katika filamu za Bongo Muvi, Shamsa Ford, ameamua kumtuliza aliyekuwa amemwandikia ujumbe mzito aliyekuwa mume wake Chidi Mapenzi, akikiri kupatana kwao tena kumempa wepesi wa moyo.

Katika ujumbe huo alioandika kupitia ukurasa wake wa Instagram, amesema kwa upande wake hana kinyongo na anatumaini wote watazikana endapo mmoja atatangulia kwa Mungu.

"Tulipoachana tulikuwa maadui wakubwa, lakini namshukuru Mungu akaweka wepesi juu yetu, mimi na wewe hatuwezi kurudiana na haitotokea tena, kila mtu ameendelea na maisha yake tumebaki ndugu wa kusaidiana," amesema.

Kisha akaendelea "Siku nilipokusamehe Mungu alinifungulia baraka nyingi mpaka nikashangaa kumbe sikujua nilikuwa najifunga nilipobeba vitu moyoni, nimeongea mengi mabaya kuhusu wewe yote ni kwa sababu ya hasira na kidonda kilikuwa kibichi."

"Namshukuru Mungu sina kinyongo na wewe tunaweza tukasalimiana tukikutana hata nife kesho najua utanizika na mimi nitakuzika, Mungu akusaidie upate mke mwema zaidi nilivyokuwa mimi akutunze inshaallah nitafurahi sana," ameongeza.



## Mwana FA aifikiria 'Slave Become A King'

MBUNGE wa Muheza ambaye ni msanii wa HipHop, Mwana Fa, ameonyesha kusikitika kutokana na kukosa kujumuishwa katika Albam ya 'Slave Become A King' ya Darassa.

"Nilitaka sana kuwamo kwenye hii album ratiba tu hazikunikubalia, nusu ya pili ya mwaka 2020 ratiba zangu zilibebwa na majukumu mengine na nimekosa kabisa muda wa kurekodi chochote, nimesikitika, lakini silalamiki kwa sababu najua 'my brother' Darassa ni mtu 'makini sana na hawezi kuniangusha, ni imani yangu tupo tayari," amesema.

Darassa amezindua album hiyo yenye nyimbo 21 ambayo ni ya kwanza tangu aingie katika muziki.

Wasanii walioshirikishwa ndani ya albam hiyo ni Dogo Janja, Billnass, Alikiba, Juma Nature, Rich Mavoko, Barakah The Prince, Ben Pol, Sho Madjozi, Maua Sama, Kassim Mganga, Eddy Kenzo na Win.



## Ngoma tano kali za kuusindikiza mwaka 2020

**Na Adam Fungamwango**

ZIMEBAKI ziku chache tu kabla ya kumalizika kwa mwaka 2020 ambao hauwezi kusahaulika si kwa Watanzania tu, bali kwa watu wote duniani.

Ni mwaka ambao vitu vingi vilisimama kutokana na ugonjwa wa COVID-19, unaosababishwa na virusi vya corona.

Hata hivyo nchini Tanzania mambo yalienda vema na baada ya miezi miwili tu, kila kitu kikakaa sawa na serikali ikaruhusu michezo yote, ikiwamo hata bendi na wasanii kufanya shughuli zao za kuwaingizia vipato.

Mwaka unamalizika, huku baadhi ya wasanii wakiusindikiza kwa kutoa ngoma kadhaa ambazo zinaonekana ni kama za kuusindikiza mwaka 2020 uende salama.

Mwezi huu Desemba baadhi ya wanamuziki wametoa ngoma zao ambazo zimeanza kusikika na kuonekana kwenye mitandao ya kijamii, televisheni na redio.

**1. AJE-ABDUL KIBA FT RICHIE REE**

Baada ya kuwa kimya kwa muda mrefu, msanii Abdul Kiba, mdogo wake Ali Kiba, ameibuka mwishoni mwa mwaka na ngoma aliyoiita 'Aje'.

Ikumbukwe kuwa kaka yake alishawahi kutoa ngoma iliyokuwa na jina hilo.

Na hata ukiisikiliza, kuna sehemu imeimbwa kama ile ya Ali Kiba mwenyewe.

Ina maana hii ni kama vile 'remix' yake. Ngoma hii imetoka Desemba 3 na kumshirikisha msanii Richie Ree.

**2. LIHAN SANGA FT DOGO JANJA**

Siku hiyo hiyo, msanii wa kike mzoefu kwenye gemu la muziki huu, Linah Sanga, aliibuka na ngoma moja kali inayoitwa 'Kilegeze'. Ni ngoma iliyoimarika kwani amemshirikisha msanii mwingine maarufu 'Dogo Janja'.

**3. SUMU BARIDI-Z ANTO**

Siku moja baadaye, baada ya wasanii hao kutoa ngoma zao, msanii Z Anto naye Desemba 4, akaja kuuaga mwaka 2020 kwa kutoa ngoma yake mpya aliyoiita 'Sumu Baridi'.

Ni wimbo wa mapenzi ambapo mwanaume anamlalamikia mpenzi wake kuwa amekuwa na mapenzi kama sumu baridi, kwani anang'ata na kupuliza.

**4. KIDANI-BEN POL**

Msanii mwimbaji mwenye sauti nzuri, Ben Pol naye hakuwa nyuma kuusindikiza mwaka 2020, kwani Desemba 9 akatoa ngoma iitwayo 'Kidani'. Anamwambia mpenzi wake ampe kidani ili iwe kama kumbukumbu au uthibitisho wa penzi lao.

**5. NALEWA LEO-STAMINA FT MAUA SAMA**

Ni ngoma ambayo imetoka Desemba 10. Kama kawaida ya Stamina kwenye mistari yake anayochana, mingi inakuwacha unacheka, mingine inakuwa na maswali mengi ya kujiuliza na mingine unabaki unashangaa tu. Kuna sehemu anachana baadhi ya wanaume ambaye wanaishi kwa kudisha nguo na magari, ili mradi tu waonekana wana pesa. Kwenye ngoma hii, Maua Sama yeye ametumika zaidi kwenye kiitikio.

## Mama Mwenye Nyumba; Utajiri wa 'mandondocha' majanga

**Na Adam Fungamwango**

BAADHI ya binadamu wamegubikwa na taamaa ya kutaka mali kwa njia ya mkato na haraka haraka. Hapa ndipo unawapata wala rushwa, mafisadi, majambazi, matapeli, wauaji na wakati mwingine hata wachawi.

Baadhi ya binadamu hawataki njia hiyo ngumu, badala yake wanapitia njia ya mkato.

Leo tunaingalia filamu ya 'Mama Mwenye Nyumba' iliyotungwa na Juma Sadiki, ambayo inaelezea jinsi baadhi ya wanavyotafuta utajiri kwa njia chafu.

Inaanza kuonyesha kuwa Mama Chaudele amepokea wageni wawili, mtu na mtoto wake. Mwanamke mmoja akiwa na mtoto wake Moyo alikuja kumtafuta baba yake.

Alidai miaka kadhaa nyuma, baba yake alifika Iringa na kumwambia kuwa anaishi hapo Kunduchi Mtonganina mama mwingine na pia kumtajia namba ya nyumba. Mama Chadele akasema hamtambui mtu huyo, lakini pamoja na hayo atawasaidia kuishi hapo kwa siku kadhaa, kumtafuta baba yake na ikishindikana kumpa nauli ya kurejea Iringa na kibinti cha kidogo, Moyo.

Kwa upande mwingine anaonekana kijana mmoja anaitwa Sam. Akiwa usingizini anatokewa na marehemu rafiki yake Frank na kumwambia kuwa anamrithisha uganga. Atakuwa na uwezo mkubwa ya kusaidia watu wenye matatizo tu na si ule uganga na kufanya kama kazi.

Nyumbani kwa mama Chaudele, wageni wake walianza kuona mauzauza ndani kiasi cha wasijue la kufanya. Siku moja mama Moyo akakutana na Sam, na alipojitambulisha kuwa anaishi kwa mama Chaudele, alimwambia kuwa mama yule si mtu mzuri, anauawa watu, ambao kwa hali ya kawaida wanaonekana wamefariki, lakini wanakuwa wanaishi na kuwafanya misukule au mandondocha kwa ajili ya kuwa tajiri na kuendelea kuzalisha itajiri zaidi na zaidi hivyo awe makini.

Pia akampa majani fulani na kumwambia akipata matatizo, basi ayafukize kwa kuyaweka kwenye moto.


Siku chache baadaye mtoto Moyo anapotea kwenye mazingira ya kutatanisha. Mama Moyo anamtuhumu mwenyeji wake kuwa amechumua msukule. Mama Chaudele, anakwenda polisi kushtaki na amakuja kukamatwa.

Kabla ya kupelekwa kituoni, mama Moyo alimtaka polisi atoe uthibitisho kama yeye si mtu mbaya.

Alichofanya ni kuchua moto na kuchoma yale majani. Mama Chaudele akaanza kulia, kwani uchawi wake ndiyo unaanza kujulikana. Ikabainika kuwa yeye ndiye aliyempoteza mtoto Moyo kwa kumuweka ndondocha, lakini pia kumbe baba ya mama Moyo naye aliwekwa msukule na mama huyo kwa ajili ya kusaka utajiri.







# Diddy ampa zawadi mama yake gari la kifahari

RAPA maarufu wa Marekani, Diddy, amefanya kufuru baada ya kumkabidhi mama yake Janice Combs, gari aina ya Bentley lenye thamani ya zaidi ya bilioni moja.

Mwanamuziki huyo milionea, amempatia zawadi hiyo mama yake wakati wa sherehe ya kutimiza miaka 80.

Video ambayo imesambaa mtandaoni, inamwonyesha rapa huyo akimkabidhi gari hilo mama yake ambaye alionekana kutoamini kile anachoshuhudia machoni mwake.



## Gucci Mane apata mtoto wa kiume

MWANAMUZIKI wa miondoko ya Hip hop kutoka Marekani, Radric Delantic Davis, ambaye anajulikana kama Gucci Mane, na mkewe Keyshia Ka'oir, wamepata mtoto wa kiume.

Staa huyo ameweka ujumbe katika ukurasa wake wa Instagram, akiwajulisha mashabiki wake kuwa ana habari njema ya kuwa hivi sasa ni baba.

"Mke wangu amenipa zawadi ya mtoto wa kiume ambaye tumemuita ICE DAVIS, asante sana !!!!!!" ameandika.


## Mr Eazi yamekutana huko Ghana

MWANAMUZIKI wa Nigeria, Mr Eazi, amekuwa gumzo katika mitandao ya kijamii baada ya kuibiwa kompyuta mpakato akiwa nchini Ghana.

Baadhi ya mastaa wa nchi hiyo wamejitokeza kumsaidia baada ya msanii huyo kuandika katika mtandao wa Twitter, akiomba watu kumsaidia kupata kumpyuta yake.

"Naomba kama kunamtu kaona kompyuta yangu huko Accra, anisaidie nitampa zawadi," amesema Mr Eazi.





## D'Banj arudi kwa kishindo Instagram

STAA wa muziki kutoka Nigeria, D'banj, ameanza kurudi katika hali yake ya kawaida baada ya watu wasiojulikana kushikilia akaunti yake ya Instagram kwa siku tano.

Wiki iliyopita, D'Banj alitangaza kuwa akaunti yake imedukuliwa na kushikiliwa na watu wasiojulikana.

"Watu wangu, asanteni sana wote kwa kuniunga mkono kwa kunipigia na kunitumia ujumbe unaonyesha kuwa na uchungu dhidi yangu," ameandika D'Banj.

## Inogie awashuhudia wasiojulikana

MWIGIZAJI maarufu kutoka Nollywood, Charles Inogie, amejikuta akikabiliana na waporaji wenye silaha akiwa katika Jiji la Logos.

Kulingana na rafiki yake wa karibu, Chinedu Ikedieze, kuwa msanii huyo apata mkasa huo wakati akiwa barabarani.

"Charles Inogie alivamiwa na waporaji wenye silaha barabarani na kumwibia simu yake ya mkononi," ameandika.





# JERUSALEM

## • Mji wa kale unaoheshimiwa na dini kuu tatu duniani

WAUMINI wa Kikristo wapo katika sherehe muhimu kwenye imani yao, ambayo ni kumbukizi ya kuzaliwa Yesu Kristo, miaka 2000 iliyopita.

Katika sherehe hiyo ya Krismasi, watu wanajumuika pamoja kwa ajili ya kula vyakula vizuri na kuvaa mavazi ya kupendeza.

Katika kipindi cha sherehe za Krismasi na Mwaka Mpya, mji wa Jerusalem ambao unaaminika ndio chimbuko la Ukristo, unakuwa na shamrashamra za kipekee.

Hata hivyo, mwaka huu sikukuu ya Krismasi katika mji huo inasherehekewa kwa ukimya kutokana na amri kali ya kupambana na virusi vya corona.

Watu hawatapata nafasi ya kwenda kujumuika na ndugu na jamaa kufurahia Krismasi, badala yake kila mmoja atasherehekea akiwa ndani ya nyumba yake na kufuata kanuni kali za kukabiliana na Covid-19.

### JERUSALEM UKO WAPI?

Mji wa Jerusalem unapatikana Mashariki ya Kati, kihistoria ndiyo mji pekee wa kale ambao watu wanaendelea kuishi hadi leo.

Hata hivyo, Jerusalem umekuwa na mzozo wa muda mrefu wa umiliki kati ya nchi ya Israeli na Palestina.

Kwa Kiebrania, Mji wa Jerusalem hufahamika kama Yerushalayim, Kiarabu al-Quds na kwa Kiswahili, huitwa Yerusalemu.

Mji huo kwa sasa huwa umegawanywa mara mbili, Jerusalem Mashariki na Jerusalem Magharibi.

Jerusalem ya Magharibi hutazamwa na Israel kama mji wake mkuu, huku Palestina inadai Jerusalem Mashariki yao na mji mkuu wa taifa lao.

Kijografia eneo kubwa la mji huo limetawaliwa na Israel tangu vita vya 1967.

Tangu kipindi hicho, Israel imejenga nyumba za walowezi wa Kiyahudi takriban 200,000 ambazo huishi Jerusalem Mashariki, hatua iliyoshutumiwa na jamii ya kimataifa. Eneo hilo wanaishi Wapalestina takriban 370,000.

Mwaka 1980 Israel ilitangaza Jerusalem yote kuwa mji wake mkuu wa milele, lakini nchi nyingi duniani hazikubali azimio hilo.

Mzozo huo umefufuliwa tena kutokana na hatua ya Rais wa Marekani, Donald Trump, kuutambua mji huo kama mji mkuu wa Israel.

Mataifa mengi ya Kiarabu yameshutumu hatua hiyo yakisema yazidisha uhasama Mashariki ya Kati.

### CHANZO CHA MGOGORO

Pamoja na mgogoro huo, bado Jerusalem unabaki kuwa mji muhimu kwa dini kuu tatu duniani za Ukristo, Uslamu na Uyahudi.

Dini zote tatu humuona Abraham au Ibrahim anayetajwa kwenye Biblia na Koran kama mmoja mwanzilishi wa imani yao.

Ni mji ambao umedhibitiwa na dini hizo kwa vipindi mbalimbali katika historia. Umetekwa, umebomolewa na kuharibiwa na kisha kujengwa tena.

Kila sehemu ya ardhi yake ukichimba kwenda chini kuna mabaki ya enzi fulani za watu waliowahi kuishi katika historia yake.

Kuna maeneo manne makuu kwenye mji huo, na hata majengo huwa tofauti. Kuna eneo la Wakristo, Waislamu, Wayahudi na Waarmenia. Eneo hilo huzungukwa na ukuta mkubwa wa mawe ambao ugawanya maeneo hayo yanayoaminika kuwa matakatifu zaidi duniani.

Kila eneo kati ya maeneo hayo manne (unaweza kuyaita mitaa) huishi watu wa aina moja. Wakristo wana maeneo mawili, kwa sababu Waarmenia pia ni Wakristo. Eneo lililotengewa Waarmenia, ambalo ndilo ndogo zaidi kati ya hao manne, lina vituo vya kale zaidi vya Waarmenia duniani.

Waarmenia wamehifadhi utamaduni wao wa kipekee ndani ya Kanisa la St James na nyumba kubwa ya utawala. Maeneo hayo mawili yamechukua sehemu kubwa ya mtaa huo wa Waarmenia.

Ndani ya Mtaa wa Wakristo, kuna Kanisa Kuu la Kaburi na Ufufuo wa Yesu Kristo, ambalo ni muhimu sana kwa Wakristo kote duniani.

Kwa mujibu wa utamaduni wa Kikristo, Yesu alisurubiwa hapo, katika Golgotha, au mlima wa Calvary. Kaburi lake linapatikana ndani ya kanisa hilo na inaaminika hapo ndipo alipofufuka.

Katika jambo la kushangaza, kanisa hilo husimamiwa kwa pamoja na madhehebu mbalimbali ya Kikristo.

Hapa ndipo mamilioni ya mahujaji wa Kikristo husafiri kila mwaka kwenda kuliona kaburi la wazi la Yesu na kutafuta ufunuo na kuomba.

Mtaa wanaoishi Waislamu inaaminika ndio mkubwa zaidi kati ya maeneo yote manne, ndani yake kunapatikana madhabahu ya Dome of Rock (Kuba ya Mwamba) na Msikiti wa al-Aqsa, ambao pia hufahamika kama Haram al-Sharif.

Msikiti huo ndio eneo la tatu kwa utakatifu katika dini ya Kiislamu na husimamiwa na wakfu wa Kiislamu ambao hufahamika kwa Kiarabu kama Waqf.

Waislamu huamini kwamba Mtume Muhammad (S.A.W) alisafiri hadi msikitini hapo kutoka Maka kwa ajili ya kufanya ziara yake maarufu ya kwenda mbinguni.

Waislamu hutembelea eneo hilo takatifu kila wakati kila mwaka, lakini kila Ijumaa wakati wa mwezi mtukufu wa Ramadhan, mamia ya malelfu ya Waislamu hufika kuomba kwenye msikiti huo.

Katika mtaa wa Wayahudi, kunapatikana Kotel, au Ukuta wa Magharibi ambao ni masalio ya ukuta wa nje uliozunguka lililokuwa Hekalu Takatifu.

Ndani ya hetalu hilo inaaminika ni eneo takatifu zaidi katika dini ya Kiyahudi.

Wayahudi huamini kwamba hapo ndipo kulikuwa na jiwe la msingi la kuumbwa kwa dunia. Ukuta wa Magharibi ni eneo la karibu zaidi ambalo Wayahudi wanaweza kufanya maombi yao.

# Corona ilivyoyumbisha chanjo Bukoba, ikarudi kwa kasi tishio

## •Kuna maeneo yenye malengo 144%

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

KATIKA sifa kadhaa zinazoibeba Manispaa ya Bukoba na hata Mkoa wa Kagera kwa jumla, ni kwamba wamepiga hatua katika mustakabali wa chanjo.

Lakini baada ya kutokea ujio wa maradhi ya Covid-19, mikakati ya chanjo iliyokuwa katika mafanikio ya juu sana, ilijikuta imeanguka kwa muda na sasa ishara ya kuibuka tena chanjo, hata ikavuka malengo yaliyopo.

Mratibu wa Chanjo Manispaa ya Bukoba, Samson Stanslaus, anasema katika kila robo ya mwaka, huwa wana malengo ya kuchanja watoto 576, lakini waliopata dozi ya kwanza katika kipindi hicho ni 48 ambao ni sawa na asilimia 8.3.

Pia, katika kukabili saratani ya mlango wa shingo ya kizazi, chanjo inawagusa mabinti wenye umri miaka 14 ya saratani ya kizazi ambao Stanslaus anasema kujitokeza kulishuka kati ya Aprili na Juni mwaka huu, Covid-19 iliopchukua nafasi.

Mratibu wa chanjo anasema, ni kawaida kila robo ya mwaka lengo lao ni kuchanja watoto 576, lakini waliopata dozi ya kwanza katika kipindi hicho ni 48 ambao ni sawa na asilimia 8.3.

Stanslaus anasema mabinti wa umri huo waliopata dozi ya pili inayotolewa baada ya kupita miezi sita tangu walipopatiwa ya kwanza ni 75, sawa na asilimia 13 ya malengo yaliyopo.




Baadhi ya kinamama wakiwa kliniki katika Kituo cha Afya Rwamishenye, katika Manispaa ya Bukoba, wakisubiri watoto wao wapatiwe chanjo.

### HODI YA CORONA

Anasema ugonjwa wa corona pia uliathiri chanjo za watoto walio na umri chini ya mwaka mmoja, akitaja takwimu waliokamilisha chanjo kati ya Aprili hadi Juni ni watoto 1,206, sawa na asilimia 74.9 ya watoto wote walengwa katika kila robo ya mwaka, ambao ni 1,611.

Anasema kabla ugonjwa wa Covid-19 kuthibitika kuingia nchini kipindi cha Januari hadi Machi mwaka huu, mabinti waliopata dozi ya kwanza kuzuia saratani ya mlango wa kizazi ni 484 sawa na asilimia 84.

"Mabinti waliopata dozi ya pili ya kuzuia saratani ni 234 ambao ni sawa na asilimia 40.6 ya lengo, pia kwa watoto wenye umri wa chini ya mwaka mmoja, waliokamilisha chanjo katika kipindi hicho ni 1,359 sawa na asilimia 84.4.

Mratibu huyo wa Chanjo, anasema takwimu zinathibitisha idadi ya watoto waliopelekwa kupata chanjo wakati wa Covid-19 ilishuka kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo wananchi kutojitokeza wakihofia maambukuzi ya corona.

Aidha, anataja wakati wa Covid-19 baadhi ya chanjo zilikosekana kutokana na ukosefu wa mgawo, baada ya ndege kutoka nchi nyingine kutoruhusiwa kuingia nchini.

"Kwa chanjo ambazo zilikuwapo mahudhurio ya wananchi hayakuwa mazuri, maana wengine walikimbia mji na kwenda vijijini, haifahamiki kama huko walikokwenda waliwapeleka watoto wao kupata chanjo au la" anasema.

### KWAHERI CORONA?

Stansalaus anasema, baada ya serikali kutangaza Covid-19 imepungua kwa kiwango kikubwa katika kipindi cha Julai hadi Septemba, idadi ya mabinti wa miaka 14 waliopata dozi ya kwanza iliongezeka hata kuvuka lengo la watoto 576.

"Waliopata dozi ya kwanza walifikia 830 sawa na asilimia 144, waliopatiwa dozi ya pili ni 368 ambao ni sawa na asilimia 64," anaeleza na kuongeza:

"Pia kwa watoto wenye umri chini ya mwaka mmoja, katika kipindi hicho waliokamilisha chanjo ni 1,423 ambao ni asilimia 88 ya lengo la robo mwaka."

Anasema, ni chanjo inayoruhusiwa kwa watoto wa umri wa miaka tisa hadi 14 na haina madhara kwa anayepungukiwa miezi michache kutimiza miaka 14.

Stanslaus anasema, ili kupima ufanisi wa dozi ya pili ya chanjo ya saratani ya mlango wa kizazi, wanasubiri upite mwaka mmoja, kwani wanaochanjwa dozi ya kwanza husubiri miezi sita, ndio wapatiwe umri huo.

Anasema, utekelezaji wa chanjo ya saratani ya mlango wa kizazi ulikumbana na kikwazo cha waliochanjwa dozi ya kwanza hawakuchanjwa ya pili, kutokana na wengi kuwa wamemaliza darasa la saba na kuondoka, hasa shule za bweni.

"Kwa sasa tumebadilisha utaratibu wa kuchanja, tutafanya kwa mfumo wa kampeni ndogo kwa kuwachanja watoto wote watakaokuwa wanatimiza miaka 14 katika mwaka husika, hata kama watakuwa wanapungukiwa miezi kadhaa, ili kuwezesha watoto kukamilisha dozi," anasema.

"Katika kampeni hii tutakuwa tunawapatia dozi ya kwanza mapema mfano mwanzoni mwa mwezi Februari, ili kufikia mwezi Julai wapatiwe dozi ya pili kabla ya kufanya mitihani ya taifa na kuondoka shuleni," anasema.

### CHANJO NYINGINE

Kwa watoto wenye umri chini ya mwaka mmoja, huongozwa na chanjo ya kuzuia maradhi ya kifua kikuu, inayotolewa mtoto anapozaliwa na kuziendeleza kwa mujibu wa kanuni, kunategemea hamasa na mwamko wa wazazi.

"Kuna wazazi wengine hawaoni umuhimu wa watoto kukamilisha chanjo zote, wanakuwa wazembe kuwapeleka watoto wao katika vituo vya kutolea huduma za afya, wanaona ni sawa, lakini wafahamu ni hatari kwa afya ya mtoto," anasema Stanslaus.

Anazitaja chanjo hizo muhimu kwa mtoto ni za kizuia Polio ya Matone (OPV); Polio ya Sindano (IPV); Surua na Rubella (MR); na Chanjo ya Kuzuia Kichomi (PCV).

Nyingine ni za kuzuia maradhi donda koo, pepopunda, kifaduro, mafua makali na homa ya ini, saratani ya mlango wa kizazi na kuzuia kuhara kunakosababishwa na kirusi aina ya rota.

### MADHARA

Stanslaus anasema, watoto kutopatiwa chanjo kuna madhara kama ya maambukizi ya magonjwa yanayozuiliwa kwa chanjo.

Anatoa mfano wa ugonjwa wa kifaduro ambao mtoto akiugua anakohoa bila kukoma, hali inayoweza kusababisha akapasuka masikio, kuwa kiziwi na hatimaye bubu.

Mratibu Chanjo anaendelea: "Hata ugonjwa wa surua unaweza kusababisha mtoto kupata mtindio wa ubongo, polio inasababisha ulemavu wa kudumu, pia magonjwa haya yote yanaweza kusababisha vifo."

Anataja jitihada za serikali kuhakikisha watoto walio kwenye umri sahihi wa kupata chanjo, wanapatiwa huduma hiyo kwa kutumia wahudumu wa afya ngazi ya jamii (WAJA), wanaozunguka kuielimisha jamii umuhimu wa watoto kuchanjwa.

"Wakifika kwenye familia wanaangalia kama kuna mtoto mwenye umri wa kupatiwa chanjo ambaye hajachanjwa, wakibainika huorodheshwa, ili kutafuta namna ya kuwafikia, hasa waasi wa chanjo," anasema.

Mratibu huyo wa chanjo ana wito kwa jamii iondokane na mila potofu, kwani chanjo zote ni salama na zimethibitishwa kiserikali.

### WAZAZI

Vicencia Patience, mkazi wa Kyakailabwa katika Manispaa ya Bukoba, ana watoto wawili, anataja uelewa umo katika sababu za wazazi kutojitokeza kupata chanjo, ikiwamo uelewa mdogo.

"Mzazi mwingine utamsikia akisema mbona watoto wa zamani walikua bila kuchanjwa. Hii ni dalili mojawapo kuwa bado elimu inahitajika kubadili mtazamo," anasema.

Pia anataja uzembe wa baadhi ya wazazi kutoa kipaumbele katika majukumu mengineyo, sambamba na wanaume kuwaachia kinamama jukumu la kupeleka mtoto kliniki.

Hata hivyo, anaunga mkono kuwapo wanaume wanaowajibika katika huduma za kliniki kwa watoto zao, pasipo kujali kejeli za kijinsia kutoka kwa wenzao.

Anatoa wito kwa wananchi wenzake kuacha uzembe unaosababisha wasiwapeleke watoto kwenye chanjo, maana kufanya hivyo kunaweza kusababisha watoto kushambuliwa na magonjwa kama surua na polio.

Katika Manispaa ya Bukoba, kuna zaidi ya Sh. milioni 14.7 zilizotengwa kuratibu masuala mbalimbali ya chanjo katika Manispaa ya Bukoba, katika mwaka wa fedha 2019/2020.



Baadhi wa watoto wakipatiwa chanjo. **PICHA ZOTE: LILIAN LUGAKINGIRA**

# Ethiopia yaua zaidi ya waasi 40

**ADIS ABABA,** ETHIOPIA

JESHI la Ethiopia limewaua zaidi ya watu 40 wanaoshukiwa kuhusika na mauaji ya raia 100 katika eneo la Benishangul-Gumuz nchini humo.

Watu waliouawa ni maofisa watano wa serikali na wenzao wa zamani.

Katika tukio lililotokea juzi, nyumba za wanavijiji zilichomwa moto wakati wamelala na kisha watu walipigwa risasi na kuwachoma visu.

Shambulio hilo lilitokea siku moja baada ya Waziri Mkuu Abiy Ahmed, kufanya ziara katika eneo hilo.

Haijulikani washambuliaji ni kina nani, lakini walionekana kulenga watu kutoka makabila madogo ambayo wamehamia eneo hilo.

Nchi hiyo imeshuhudia ongezeko la ghasia za kisiasa, kikabila na kidini katika miaka ya hivi karibuni.

Waziri Mkuu alisema mauaji hayo yanasikitisha na kueleza kuwa serikali yake imetuma wanajeshi katika eneo hilo, ili kutafuta suluhu ya mzozo huo.

Naibu waziri wa serikali ni miongoni mwa watu watano waliokamatwa, vilisema vyombo vya habari vya serikali.

Miongoni mwa watu hao, watano walidaiwa kuhusika na tukio hilo, huku wengine walikamatwa kwa sababu hawachukua hatua ya kuzuia mauaji hayo.

Msemaji wa Tume ya Haki za Kibinadamu inayoendeshwa na serikali ya Ethiopia, aliambia BBC, kuwa wapiganaji walitekeleza shambulio hilo katika eneo la magharibi mwa Benishangul-Gamuz.

"Walivamia kijiji kimoja wakati watu wakiwa wamelala, walizichoma nyumba zao na pia waliwapiga risasi raia," alisema Aaron Maasho.

**BBC**



Kiongozi wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis, aliongoza mkesha wa sikukuu ya Krismasi katika Kanisa la St. Peter's Basilica, mjini Vatican, jana. **PICHA AFP**

# Sherehe ya Krismasi yatanda hofu Covid-19

**VATCAN,** ITALIA

WAUMINI wa dini ya kikristo wanaadhimisha sikukuu ya Krismasi ya kuzaliwa kwa Yesu Kristo, katika hali ya tahadhari kutokana na janga la virusi vya corona linalozidi kuangamiza maisha ya watu duniani.

Kiongozi Mkuu wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis, alitoa tamko la kuwataka waumini wa kanisa hilo, kufuata maagizo yote ya mamlaka za kiserikali ili kuzuia kusambaa kwa virusi vya corona.

Kiongozi wa kiroho wa kanisa hilo kwenye Ukingo wa Magharibi, Pierbattista Pizzaballa, alitumia ibada ya Mkesha wa Krismasi kuiombea dunia iondokane na janga hilo.

Kiongozi huyo alilazimika kuendesha misa ya Mkesha wa Krismasi mbele ya viongozi wa kidini pekee mjini Bethlehem, ambako inaaminika ndiko alikozaliwa Yesu Kristo.

Rais Mahmoud Abbas wa Palestina, ambaye kawaida huhudhuria maadhimisho hayo, safari hii ameshindwa kufika kwenye Kanisa la Nativity kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2005.

Ukingo wa Magharibi umeweka kwenye marufuku ya kutotoka nje kuanzia saa moja usiku hadi 12 asubuhi kwa wiki kadhaa sasa, ili kukabiliana na kasi ya maambukizo ya virusi vya corona.

Eneo hilo linalokaliwa na Wapalestina milioni 4, limeshapoteza watu 800 hadi sasa kutokana na ugonjwa wa COVID-19.

Sherehe ya Krismasi itafanyika bila mikusanyiko kama iliyozoeleka katika maeneo mbalimbali duniani kutokana na hofu ya kueneza maambukizi.

Waumini wa Kikristo nchini Australia, walitakiwa kununua tiketi mtandaoni, ili kushiriki misa katika kanisani mbalimbali, lakini kwa kufuata kanuni ya kukaa mbali.

Ufilipino imepiga marufuku mikusanyiko mikubwa na vikao vya familia katika mkesha wa Krismasi.

Nchini Ugiriki, ambako kawaida watoto huwa wanapita nyumba kwa nyumba kutoa mkono wa kheri ya Krismasi, shughuli hiyo ambayo ni kama mila imesitishwa.

Katika mkesha wa Krismasi, huko nchini Italia, kengele za makanisani zililia mapema kuliko kawaida.

Hali hiyo inatokana na hatua ya serikali kupiga marufuku watu kutotoka nje kuanzia saa nne usiku, hivyo viongozi wa makanisa wakapanga sherehe ya mkesha kuanza mapema.

Hata ibada maalum ya Krismasi kwenye uwanja maarufu wa Mtakatifu Petro, Basilica, ilirudishwa nyuma badala ya saa tatu na nusu usiku kama inavyofanyika miaka yote.

**DW**

## Waasi Afrika ya Kati wasitisha vita

**BANGUI,** AFRIKA YA KATI

MUUNGANO wa waasi katika Jamhuri ya Afrika ya Kati, ambao unapigana na serikali, umesema utasitisha mapigano kwa siku tatu, kuelekea uchaguzi mkuu utakaofanyika kesho.

Uchaguzi huo unatazamwa kuwa mtihani kwa taifa hilo, linalozongwa na migogoro ya kikabila na kidini.

Taarifa iliyotolewa na wanamgambo hao wanaoitwa Muungano wa Wazalendo wa Mabadiliko (CPC), ilisema wapiganaji wake wote watasitisha vita kwa saa 72 nchini kote.

Makundi mawili kwenye muungano huo wa CPC, yamelithibitishia shirika la habari la AFP, kuwa taarifa hiyo ni kweli.

Muungano wa CPC uliundwa Desemba 19 na makundi yenye silaha ambayo yanamtuhumu Rais Faustin Archange Touadera, kuwa na njama ya udanganyifu kwenye uchaguzi huo.

**DW**

## Makombora ya Israeli yaua sita Syria

**DAMASCUS,** SYRIA

WAPIGANAJI sita wenye mfungamano na Iran, wameuawa katika eneo la kati la Syria, kufuatia mashambulizi ya makombora yaliyofanywa na Israel.

Kulingana na shirika linalochunguza haki za binadamu nchini Syria, limesema shambulizi hilo lililofanyika asubuhi ya jana katika mkoa wa Hama, na kusababisha uharibifu wa maghala na viwanda vya kutengeneza makombora vinavyomilikiwa na wanamgambo hao.

Shirika rasmi la habari linalomilikiwa na serikali ya Syria SANA, liliripoti kuwa makombora ya Israel yalilenga eneo la Masyaf mkoani Hama.

Shirika hilo lilinukuu duru ya kijeshi na kuongeza kwamba Jeshi la anga la Syria lilifanikiwa kuyadungua makombora kadhaa yaliyofyatuliwa.

**DW**

# HABARI PICHA



Viongozi wa Kanisa la Glory Temple Tanga, wakigawa zawadi kwa watu wenye mahitaji maalumu, wakiwamo wenye ulemavu, wazee, wajane na waathiriwa wa dawa za kulevya kanisani hapo, ikiwa ni sehemu ya kusherehekea sikukuu ya Krismasi jana. **PICHA: BONIFACE GIDEON.**



Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Khamis Hamza Chilo, akitoa sadaka kwa watoto baada ya kumalizika kwa ibada ya Krismasi iliyofanyika jana, katika Kanisa Katoliki Parokia ya Kiboje, Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, akifafanua jambo jana, alipokuwa ziarani Wilaya ya Mwanga mkoani Kilimanjaro, kukagua mradi mkubwa wa maji utakaohudumia Wilaya za Mwanga, Same na Korogwe. Aweso amemsimamisha kazi mkandarasi M.A Kharafi & Sons anayetekeleza mradi huo kutokana na kushindwa kukamilisha kazi hiyo. **PICHA: GODFREY MUSHI**



Baadhi ya waumini wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Kanisa Kuu Iringa, wakisalimiana kwa kupungiana mikono wakati wa mkesha wa Krismasi juzi usiku. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

**HADITHI**

# HADITHI

MAUAJI ya kutisha yanatokea ndani ya gesti moja maeneo ya Kigogo jijini Dar es Salaam.  Mfanyabiashara Burhan anauawa ndani ya gesti ya Tukutane, akiwa na msichana mmoja mrembo aitwaye Mwanaidi. Polisi wanawakamata watu wote waliokutwa humo, pamoja na wafanyakazi wa gesti hiyo kwa ajili ya mahojiano. Lakini inaonekana muda ambao walikuwapo wapenzi hao hakukuwa na mteja mwingine yeyote zaidi yao.

Baada ya mahojiano ya kina, inaonekana kabisa kuwa Mwanaidi ndiyo muuaji. Je, ni kweli? Kwa nini alimuua mpenzi wake wakiwa wamejifungia chumbani? Fuatilia hadithi hii kwa makini ambayo mbali na kukutia simanzi, furaha na kukuburudisha, pia itakufundisha, elimu na kufunulia mambo ambayo hukupata kuyafikiria kabla.

# Lazima Apatikane - 1

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

"Nakuuliza mara ya mwisho. Wewe ndiye uliyemuua Burhan?"

Safari hii Inspekta Kenneth Msiya alionekana mkali kwa msichana anayemhoji. Aliinamisha kichwa chake kwenye meza ya ofisi. Akaangua kilio cha kwikwi.

Alimuacha kwanza alie. Alikuwa na uelewa kuwa kulia humfanya mtu apunguze hasira, au machungu aliyonayo. Dakika mbili baadaye, msichana aliinua kichwa. Macho yalikuwa yamevimba.

Ilionekana kutokana na kulia na kutopata usingizi wa kutosha.

"Afande mimi sijui niseme nini? Na niseme mara ngapi? Mimi sijaua jamani?"

Inspekta Msiya alimtazama tena msichana huyo kwa makini.

Akashusha pumzi. Kuna kitu kama anakiona kwenye sura ya msichana huyo. Sura ya maumivu na ya kutaka kuonewa huruma. Lakini Inspekta Msiya hakuweza kufanya hivyo.

Msichana huyo alikuwa ameua. Amemuua mpenzi wake kwenye nyumba ya kulala wageni.

Hakuna chochote kinachoweza kumsalimisha, au kumpunguzia adhabu inayomkabili.

"Hebu niambie Mwanaidi, hivi wewe unadhani nani amemuua Burhan wakati wewe ulikuwa ndani na mmejifungia?" Aliuliza Inspekta Msiya.

"Kusema kweli sijui niseme nini afande. Sema majanga yakitaka kukupata yatakupata tu afande. Mimi nilitoka kidogo kwenda kununua soda dukani tena alinituma mwenyewe marehemu, na wala hakukuwa mbali na pale, dakika kumi tu, niliporudi na kuingia ndani nilichokikuta ndugu afande siwezi kusahau kwenye maisha yangu. Burhan alikuwa amelala kitandani kukiwa na dimbwi la damu. Alikuwa amepigwa kisu na kilikuwa kimeachwa pale pale kimening'inia. Akili zikaniruka hapo hapo, nikazimia." Mwanaidi alisema na kuinamisha tena kichwa chake, akaanza kulia kwa mara nyingine.

"Sikiliza Mwanaidi. Kulia hakutokusaidia. Hii ni kesi ya mauaji. Na adhabu yake ni kunyong'a hadi kufa. Kama si hivyo, basi unaweza kufungwa maisha. Lakini kama ukinieleza ukweli kuwa wewe umeua na sababu za kumuua mpenzi wako, basi mahakama inaweza kukupunguzia adhabu, ukafungwa hata miaka mitatu au




**Labda alikuwa mpenzi wako, kuna kitu ambacho kilikukera sana ndiyo maana ulipatwa na hasira, ukaamua kumuua, au huko nyuma alishawahi kukukatisha masomo yako, akakutoroka ukakutana naye akawa amekusahau, unajua sisi binadamu tuna mambo mengi ya kukwazana.**

mitano hivi." Inspekta Msiya alisema ikiwa ni nia ya kulainisha Mwanaidi aseme ukweli, badala ya ile ya vijana wake kumpa adhabu kushindikana.

"Kwani afande wewe unataka niongee vipi?"

"Labda alikuwa mpenzi wako, kuna kitu ambacho kilikukera sana ndiyo maana ulipatwa na hasira, ukaamua kumuua, au huko nyuma alishawahi kukukatisha masomo yako, akakutoroka ukakutana naye akawa amekusahau, unajua sisi binadamu tuna mambo mengi ya kukwazana."

Mwanaidi aliinua macho na kumtazama usoni Inspekta Msiya. Alisoma macho yake kama mtu ambaye anataka kumlainisha ili akubali na kupata kile walichokuwa wakikihitaji kabla ya kufungua jalada na kulipeleka mahakamani.

Lakini alimuona kama vile askari huyo ana huruma fulani kwake, kuliko wale vijana wake, askari wa kike ambao walimpa adhabu kali ili kumfanya aseme kweli, lakini ilishindikana alipowaambia kuwa yupo tayari kufa, lakini hawezi kusema kama amemuua Burhan. Ni kweli. Lengo la Inspekta Msiya lilikuwa ni hilo. Ni kutaka kupata ukweli ni kumsaidia binti huyo.

Chochote atakachosema kuwa hajamuua Burhan, hakuna ulimwengu utakaomwelewa. Ni yeye ndiye aliyekwenda naye hadi gesti. Na wote waliandikisha kwenye kitabu, ingawa majina yalikuwa si halisi.

Lakini waliingia chumbani wawili. Hakuna yeyote aliyeonekana zaidi yake ambaye alikuwa amezirai chini ya kitanda, huku marehemu akiwa amelala kitandani.

"Sasa kama wewe hukumuua, nani ataamini wakati mlikuwa wote?"

"Hakuna atakayeamini." Mwanaidi alijibu kirahisi tu na ilionekana kama vile kijeuri.

"Unaanza kunijibu jeuri eee?" Inspekta alifoka.

"Hapana Inspekta, nimesema hivyo kwa nia nzuri tu. Ni kwamba kwa jinsi mazingira yalivyo, sidhani kama kuna binadamu yeyote anaweza kuniamini mimi nikisema sijamuua Burhan. Burhan ni mpenzi wangu. Na nilikutana naye mwezi mmoja tu uliopita. Kusema kweli alionekana kunipenda, japo yeye nilijua kabisa si mkaaji sana hapa. Aliniambia ni mfanyabiashara amekuja tu kuchukua mzigo na kuondoka. Lakini akaniambia atanifuata tena aje kunichukua anipeleke Mwanza."

"Sasa wewe unadhani ni kitu gani kimetokea hadi ameuawa kama siyo wewe?"

"Afande mimi mwenyewe nashangaa kilichotokea. Kusema kweli ni tukio la ajabu ambalo siwezi kulihadithia, ndiyo maana nakwambia siwezi kusema eti nimemuua ili nije na sababu ambazo zitanipunguzia adhabu wakati mimi sijamuua. Bora hivi ninavyokataa, kama nyinyi mkiona nimemuua sawa tu."

"Sisi tutaandika na kuipeleka kesi hii mahakamani, lakini jinsi ilivyo, ushahidi wote unaonekana kuwa wewe ndiyo muuaji, huwezi kukwepa hilo."

"Najua. Ndiyo maana nimesema kuwa mimi nimekuwa binadamu mwenye bahati mbaya sana duniani. Nimempata mwanaume ambaye nilijua shida zangu zote na matatizo yangu yote yameisha, lakini leo yametokea haya. Pesa alizokuwa ananipa ni nyingi sana na sijawahi kuzipata kwa mwanaume yoyote yule, nisingeweza kumuua, ila kumlinda. Na kwa sababu Burhan amekufa, mimi pia nipo tayari kunyongwa hadi kufa."

Inspekta Msiya alitabasamu kidogo akamuuliza "Kama uko tayari kunyongwa kwa sababu ya mpenzi wako kwa nini usikubali tu kuwa umemuua ili urahisishe kazi?"

"Hapana, siwezi kudanganya ili ninyongwe. Na siwezi kusema kwa mdomo wangu huu kuwa nimemuua mpenzi wangu niliyempenda wakati si kweli."

Inspekta Msiya wa Polisi Makao Makuu, ndiye aliyepewa kusimamia jalada kwa ajili ya upelelezi na kuchukua maelezo ya mtuhumiwa kabla ya kulipeleka mahakamani.

Mwanaidi alikaa kituoni kwa wiki moja, kwanza ikiwa akili yake ikae sawa kutokana na sakata lenyewe jinsi lilivyo kwani alikuwa amezirai kwenye tukio hilo, lakini ni kutaka kuchukua maelezo yenye kina na yenye uhalisia na si ya kudhani kwa sababu ilikuwa ni kesi nzito ya mauaji.

"Ni kweli ulikuwa unampenda Burhan?"

"Ndiyo afande."

"Kwa nini?"

"Kwanza alionekana kunipenda sana. Lakini alikuwa ananijali na kunipa pesa kwa kiasi ninachohitaji, kiasi kwamba nimeweza hata kumtumia mama Singida akanunua kiwanja na kama ningeendelea naye nina imani ningejenga."

Aliinua simu na kumuita Koplo Hamisi. "Mchukue mpeleke kwenye kile chumba halafu urudi hapa."

Dakika tano baadaye Koplo Hamisi alirejea kwa bosi wake Inspekta Msiya.

"Huyu msichana bado anakataa kuwa yeye hajaua. Najua ameua ila hawezi kukubali, kwa sababu mazingira yote yanaonyesha kuwa yeye ndiyo muuaji."

"Ni kweli Inspekta, kila kitu kinaonyesha hivyo. Hakukuwa na mtu yoyote kwenye gesti hiyo kwa wakati huo. Ulikuwa ni mchana ambapo mara nyingi huwa hakuna wateja wengi. Msichana wa zamu wa kaunta ambaye tulimkamata mwanzo, anasema hakukuwa na wateja wengine zaidi yao na hakuna mtu yeyote zaidi yao. Afande asitupotezee muda ni wakati sasa wa kuipeleka mahakamani." Koplo Hamisi alishauri.

"Sawa leo ni Ijumaa, ikifika Jumatatu asubuhi, litakuwa tayari limeshakamilika kwa ajili ya kupeleka mahakamani. Ila kwa kumsaidia, kifungu kiwe kuua bila kukusudia, sasa huko mbele kwenye ushahidi ndiyo itajulikana kama aliua kwa kukusudia au la."

"Sawa afande."

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

## HABARI MICHEZO



# RASHFORD KUONGEZEWA MKATABA MPYA

**MANCHESTER,** England

STRAIKA wa Manchester United, Marcus Rashford anakaribia kupewa mkataba mpya pale Old Trafford.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 22, mkataba wake wa sasa na United unamalizika mwaka 2024, na Mashetani Wekundu hao wapo mbioni kumwongezea mkataba mapema mwakani kabla ya mashindano ya Euro kuanza.

Kwa sasa Rashford anapokea mshahara wa pauni 200,000 kwa wiki na mkataba mpya utamfanya kijana huyu kuongezewa mshahara wake maradufu.

Hii inatokana na kiwango kizuri anachokionyesha ndani ya uwanja akiwa tayari ameshazifumania nyavu mara 12 msimu huu.

Nje ya uwanja, Rashford amekuwa ni mfano wa kuigwa na jamii kutokana na harakati zake za kusaidia watoto nchini Uingereza.

Kwa mujibu wa ripoti, United imeamua kumwongezea mkataba baada ya klabu kadhaa kumnyemelea Rashford.

United wanalenga kuongeza mkataba wa mshambuliaji huyo na kumpatia nafasi zaidi kocha, Ole Gunnar Solskjaer kuendelea na mipango yake ya muda mrefu.

Real Madrid, Barcelona na PSG ni miongoni mwa klabu zinazotajwa kuvizia saini ya Rashford.

# Pochettino anukia kubeba mikoba PSG

**PARIS,** Ufaransa

MAZUNGUMZO yanaendelea kati ya Paris Saint-Germain na aliyekuwa kocha wa Tottenham Hotspur, Mauricio Pochettino na yapo katika hatua kubwa.

Thomas Tuchel alitimuliwa na PSG juzi Alhamisi, miezi minne baada ya kuipeleka PSG katika Fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mazungumzo baina ya aliyekuwa kocha wa Tottenham, Southampton na Espanyol, Pochettino yanaaminika kuwa katika hatua za mwisho, huku ikisubiri kuafikiana na makubaliano kwa pande zote.

Pochettino ambaye alitimuliwa Spurs Novemba, mwaka jana, anatarajiwa kuwashinda Thiago Motta, ambaye PSG wamekuwa wakiwasiliana naye hivi karibuni kwa ajili ya kibarua hicho.

Kufukuzwa kwa Tuchel kunakuja baada ya kutoa kauli ambayo ilichukuliwa kama kukosa adabu kwa viongozi wa klabu hiyo.

"Tumepoteza wachezaji wengi ambao walikuwa huru (bila mikataba). Imekuwa zaidi. Hatuwezi kupata tulichokipata katika msimu uliopita katika kikosi hichi," alisema Tuchel.

Siku iliyofuata Mkurugenzi wa Michezo, Leonardo alitoa kauli ambayo ilionekana dhahiri kuchukizwa na maneno ya Tuchel.

"Inabidi uheshimu watu walioko juu yako, sijapenda kauli yake na klabu haijapenda pia," alisema Leonardo.





# *Klopp: Hatutamwahisha Alcantara*

**LIVERPOOL,** England

THIAGO Alcantara hatarejeshwa mapema kuanza kucheza licha ya kurejea kufanya mazoezi na kikosi cha kwanza, kwa mujibu wa Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp.

Nyota huyu raia wa Hispania ameshindwa kuwapo dimbani kwa zaidi ya miezi miwili sasa tangu alipopatikana na jeraha la goti kwenye dabi ya Merseyside dhidi ya Everton, Oktoba, mwaka huu.

Nyota huyu pia alipatikana na maambukizi ya corona, kitu kilichomfanya akose mechi nyingi zaidi.

Amecheza mara mbili tu akiwa na klabu ya Liverpool tangu alipowasili klabuni hapo akitokea Bayern Munich. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 29 amerejea kufanya mazoezi na kikosi kizima cha timu ya Liverpool, mapema Jumatano.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Klopp, kumchezesha kwenye mechi Jumapili dhidi ya West Brom bado itakuwa ni mapema sana kwa nyota huyu kurejea dimbani.

Klopp anaamini Xherdan Shaqiri na James Milner wanaweza wakarejea na kuwa msaada wakati Alcantara akiendelea kusubiri.

## HABARI MICHEZO

# Benzema ataka mafanikio zaidi

**MADRID,** Hispania

KARIM Benzema nyota wa kikosi cha Real Madrid amesema atazidi kupambana ndani ya uwanja ili kufikia mafanikio ambayo anayahitaji.

Ndani ya LaLiga, Benzema ni miongoni mwa wachezaji wakali watatu wa kutupia nyavuni huku akimpoteza nyota wa Barcelona, Lionel Messi.

Benzema akiwa amecheza mechi 13 ametupia jumla ya mabao nane na kutoa pasi tano za mwisho, huku akiwa amepiga jumla ya mashuti 33.

Wengine wenye mabao nane ni Iago Aspas wa Celta Vigo na ana pasi tano pia za mabao akiwa amecheza mechi 15 na Gerard Moreno wa Villarreal ametoa pasi moja ya bao na amecheza mechi 13.

Luis Suarez wa Atletico Madrid ametupia mabao saba akiwa amecheza mechi 10, huku Messi wa Barcelona akiwa ametupia mabao saba na pasi moja ya bao kwenye mechi 14 alizocheza.

Benzema ambaye amekuwa haimbwi sana licha ya jitihada zake ndani ya uwanja amesema: "Nitazidi kupambana daima, nina amini kwamba mafanikio hayawezi kuja ikiwa nitashindwa kuongeza juhudi.

"Naamini malengo yangu yatatimia tu, kikubwa ni kwamba nataka kupambana zaidi uwanjani kwa sasa," alisema akinukuliwa na gazeti la AS.






# OZIL: ARSENAL 'WANAMMISI' SANA WENGER

**LONDON,** England

MESUT Ozil anaamini Arsenal 'wanammisi' sana kocha wa zamani wa klabu hiyo, Arsene Wenger.

Mfaransa huyo, ambaye alishinda mataji matatu ya Ligi Kuu England alimaliza kipindi chake cha miaka 22 na washikabunduki hao Mei, 2018.

Mrithi wake Unai Emery alifutwa kazi mnamo Novemba, 2019 na kocha wa sasa, Mikel Arteta anawindwa na jinamizi hilo hilo.

Kwa sasa Arsenal wapo nafasi ya 15 kwenye msimamo wa ligi, na kibarua cha Arteta kipo mashakani.

Hali inaweza kuwa mbaya zaidi ikiwa hawatachukua hatua chanya haraka, Arteta amekuwa akisisitiza mipango yake ya kufanya mabadiliko na kurejea kwenye nafasi yao.

Wakati Arteta akiwa kama kocha, Ozil alitemwa kwenye kikosi chake cha wachezaji 25 wa Ligi Kuu England msimu huu, licha ya mchezaji huyo wa Ujerumani kulipwa mshahara mkubwa wa pauni 350,000 kwa wiki.

Katika mahojiano ya maswali na majibu kwenye ukurasa wake wa Twitter, Ozil, ambaye hajaichezea Arsenal tangu Machi mwaka huu, aliulizwa ikiwa alimwona Wenger kama 'baba kwake.'

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 alijibu: "Alikuwa kocha mzuri sana. Ndiyo, pia alikuwa ni kama baba kwangu na wachezaji wengine wengi.

"Nadhani watu wengi karibu na Arsenal wanamkumbuka. Ni wakati mgumu sana kwa kila mtu wa karibu na klabu - sio kwangu tu. Hali hiyo inakatisha tamaa kwa kila mtu."

Lakini nyota huyu alipoulizwa kama anafurahia kuwapo klabuni hapo alijibu: "Kwa kweli ningetamani kama ningeweza kuisaidia timu hasa kipindi kama hiki, lakini kwakuwa sipati nafasi natumaini tutapata matokeo bora mapema sana."

# *Wakala wa Isco awaita Arsenal*

**LONDON,** England

WAKALA wa Isco anayekipiga katika timu ya Real Madrid, Parco Alarcon ameitaka klabu ya Arsenal kujipanga kama inataka huduma ya mchezaji huyo.

Alcon amekiri kuwa mchezaji huyo ana mpango wa kucheza nje ya LaLiga na kuitaka klabu hiyo, kujipanga kama inataka huduma ya mchezaji huyo.

Isco amekuwa akihusishwa sana na mpango wa kuondoka Real Madrid kwa madai kwamba hana furaha ndani ya klabu hiyo.

Arsenal imekuwa ikitajwa kuwa ni moja ya klabu inayomnyatia mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania.

Na wakala wake, Alarcon ameiambia AS kwamba, kama Arsenal wanamtaka mchezaji huyo wanatakiwa kuweka mezani ofa yao.

"Nimesikia, lakini sijapata ofa yoyote kutoka kwa Arsenal, lakini kama wanamuhitaji wanatakiwa kuja mezani," amesema wakala huyo.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI AFICHUA SIRI KUTONG'ARA LALIGA

**Mshambuliaji huyo asema aliathirika kiakili baada ya mchakato wa kuondoka Barca...**

**BARCELONA,** Hispania

NAHODHA wa Barcelona, Lionel Messi, amefichua siri ya kushindwa kuonyesha kiwango maridhawa msimu huu, na kuisaidia klabu hiyo kuwa tishio kama ilivyozoeleka, kulingana na matokeo ya misimu iliyopita.

**Messi amesema jaribio lake la kutaka kuondoka klabuni hapo ambalo liligonga mwamba wakati wa usajili wa majira ya joto mwaka huu, limemwathiri kwa kiasi kikubwa.**

Agosti, mwaka huu, mshambuliaji huyo kutoka nchini Argentina alidhamiria kutumia kifungu cha sheria katika mkataba wake, ambacho kingemwezesha kuondoka katika klabu hiyo, lakini viongozi wa Barcelona walikataa, kwa kuweka wazi endapo angeondoka ada yake ya uhamisho ilipaswa kuwa euro milioni 700.

"Nilivuta kila kitu hadi mwanzo wa msimu," amesema Messi mwenye umri wa miaka 33, alipohojiwa na kituo cha televisheni cha Hispania cha La Sexta.

"Ukweli ni kwamba sasa sina neno, lakini dirisha la uhamisho lililopita lilikuwa ni wakati mbaya sana."

Hata hivyo Messi, anaweza kuondoka Barcelona bila malipo mkataba wake utakapokamilika mwisho wa msimu huu, na atakuwa na uwezo wa kujadiliana na klabu nyingine kuanzia Januari, Mosi mwakani.

Rais wa mpito wa Barcelona, Carlos Tusquets, ambaye alichukua nafasi ya uongozi wa klabu hiyo hadi uchaguzi utakapofanyika mwezi ujao baada ya Josep Maria Bartomeu kujiuzulu Oktoba, mwaka huu amesema:

"Kulingana na tathmini ya kifedha, Messi angekuwa ameuzwa katika dirisha la uhamisho lililopita."

Wachezaji wa FC Barcelona walikubali kupunguziwa marupurupu Novemba, mwaka huu, ili kuwawezesha washindi hao mara 26 wa taji la LaLiga kuokoa euro milioni 122.

"Kwa sasa najihisi vyema na natarajia kukabiliana vilivyo kushinda katika kila shindano lililopo mbele yetu. Nafahamu klabu inakabiliwa na hali ngumu kwa sasa katika ngazi ya usimamizi, uwanjani na kila kitu kinachozunguka Barca kwa sasa ni kigumu, lakini najihisi mwenye furaha," alisema Messi.

## ZISIKUPITE

### MBAPPE NA MADRID

KUFUKUZWA kazi kwa Kocha wa PSG, Thomas Tuchel, kumeathiri matumaini ya klabu ya Real Madrid kumsajili mshambuliaji, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 21 kutoka klabu hiyo ya Ligue 1.***(AS)***

### MAITLAND-NILES SOKONI

KLABU ya Atletico Madrid inajaribu kumsajili beki wa Arsenal na Timu ya Taifa ya England mwenye umri wa miaka 23, Ainsley Maitland-Niles kwa mkopo ifikapo Januari mwakani. ***(Mail)***

### ALONSO ANUKIA ATLETICO

MLINZI wa kushoto wa Chelsea, Marcos Alonso anatajwa kuwindwa na Atletico Madrid, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 akikosa fursa ya kukichezea kikosi cha kwanza cha timu hiyo ya Stamford Bridge msimu huu. ***(El Chiringuito, via Football London)***

### SOLSKJAER ASAKA BEKI

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer anataka kumsajili mlinzi wa kati mwakani, lakini hatajiunga katika kinyang'anyiro cha kumwania beki wa Austria, David Alaba (28), ambaye mkataba wake unamalizika mwisho wa msimu. ***(Telegraph - subscription required)***

### PIOLI AMTULIZA CALHANOGLU

KOCHA wa AC Milan, Stefano Pioli anamtaka kiungo wa kati wa Uturuki, Hakan Calhanoglu, ambaye amehusishwa na Manchester United kusalia katika klabu hiyo huku mazungumzo kuhusu mkataba mpya yakiendelea. ***(Goal)***

### DE ROON MAWINDONI

KLABU za Manchester City na Tottenham Hotspur zinamchunguza kiungo wa kati wa klabu ya Atalanta na Uholanzi mwenye umri wa miaka 29, Marten de Roon, ambaye aliwahi kuichezea Middlesbrough. ***(90 Min)***

### TOSUN AKATALIWA

KOCHA wa Feyenoord, Dick Advocaat amefutilia mbali hatua ya kutaka kumnunua mshambuliaji wa Everton na Uturuki, Cenk Tosun mwenye umri wa miaka 29. ***(FC Update, via Sport Witness)***

### SHKODRAN BADO SANA

BARCELONA imepinga madai kwamba ina nia ya kumsajili beki wa Arsenal na Timu ya Taifa ya Ujerumani mwenye umri wa miaka 28, Shkodran Mustafi. ***(Mundo Deportivo, via Mail)***

### CHELSEA, UNITED VITANI

CHELSEA imejiunga na Manchester United katika mbio za kuwania kumsajili kiungo wa kati wa Ecuador, Moises Caicedo mwenye umri wa miaka 19, anayeichezea klabu ya Independiente del Valle. ***(Mail)***

### NAPOLI KUMUUZA RUIZ

KLABU ya Napoli itasikiliza ofa kwa kiungo wa kati wa Hispania, Fabian Ruiz baada ya mazungumzo kuhusu mkataba mpya na mchezaji huyo kugonga mwamba. ***(Calciomercato, via Football Italia)***

## HABARI MICHEZO

## Tenisi vijana U-17 kuchuana Februari

**Na Shufaa Lyimo**

KATIKA kuhakikisha timu yake inafanya vyema kwenye mashindano ya vijana ya tenisi ya umri chini ya miaka 17, Kocha Mkuu wa Klabu ya Gymkhana, Salum Mvita, amesema kikosi chake kinaendelea kujifua wakati wote, imefahamika.

Mashindano ya Taifa ya Vijana ya U-17 ya mchezo yanatarajiwa kufanyika mapema Februari, mwakani hapa jijini, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mvita alisema ameamua kuendelea kuwapa mazoezi wachezaji wake, ili kuwaweka sawa na kuelekea mashindano hayo.

Mvita alisema kwa muda mrefu mwaka huu wachezaji wake walikuwa nyumbani kufuatia kuwapo kwa ugonjwa wa corona, hivyo wanalazimika kufidia muda ambao hawakufanya mazoezi.

"Kwa sasa tunaendelea na mazoezi kwa wachezaji ambao wanajiandaa na mashindano ya vijana yaliyopangwa kufanyika mapema mwakani, tunataka kuwa na kikosi imara kitakachotuwakilisha vizuri," alisema Mvita.

Kocha huyo aliwataka wazazi kuwaruhusu watoto kujiunga na mchezo huo ambao kipindi cha nyuma ulionekana unachezwa na familia zenye uwezo wa juu, jambo ambalo si kweli.

"Miaka ya sasa mchezo wa tenisi umekuwa kwa kasi, ni jambo ambalo linaleta faraja kwa upande wetu sisi makocha na viongozi, umebadilisha taswira iliyokuwapo," Mvita alisema.

## Majeruhi chanzo JKT 'kupepesuka'

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa JKT Tanzania, Mohamed Abdallah 'Bares' amesema matokeo mabaya waliyopata katika baadhi ya mechi za mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Bara yalitokana na kikosi chake kuathiriwa na majeruhi wengi.

Bares alitoa kauli hiyo baada ya kumaliza mzunguko wa pili kwa kupata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya KMC, katika mechi iliyochezwa kwenye uwanja wake wa nyumbani wa Jamhuri ulioko jijini Dodoma.

Kocha huyo alisema matokeo hayo yasiyopendeza hawajayatarajia na pia yaliwashangaza mashabiki wake waliokuwa wanaifuatilia timu hiyo.

"Mzunguko wa kwanza umemalizika, tumeshinda kwenye mechi hii ya mwisho dhidi ya KMC, asante wachezaji wangu kwa kupambana, lakini niseme tu mzunguko wote wa kwanza haukuwa mzuri kwa sababu kikosi kilitawaliwa sana na majeruhi, ndiyo maana utaona hatukufanya vizuri," alisema Bares.

Hata hivyo alisema baadhi ya wachezaji wake waliokuwa majeruhi wameshaanza kupona na kurejea kwenye kikosi, hivyo wanatarajia kurejea katika ushindani.

JKT Tanzania yenye pointi 17, imemaliza mzunguko wa kwanza ikiwa katika nafasi ya 15 baada ya kushinda mechi nne, kutoka sare tano na kupoteza mechi nane, imefunga mabao 17 na kuruhusu nyavu zao kutikiswa mara 20.

# MAPOKEZI UWANJA WA NDEGE YAMELIPA - YANGA

**Na Adam Fungamwango**

UONGOZI wa Yanga umesema uamuzi wa wanachama na mashabiki wa timu yao kuwapokea wachezaji wapya wa kimataifa kwenye Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam, walipokuwa wanawasili nchini haukufanyika kwa bahati mbaya na sasa matunda yake yanaonekana.

Akizungumzia tathmini ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa timu yao, Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema lengo la mapokezi yale ilikuwa ni la kimkakati na nia ni kuwafanya wachezaji hao watambue wanakuja kutumikia timu yenye kiu ya mafanikio.

Bumbuli alisema dhamira yao kubwa ilikuwa ni kuwapa ujumbe kwamba Yanga inahitaji kufanya vyema, ni timu kubwa na yenye heshima.

**Alisema matokeo ya mapokezi hayo yameshapatikana kwa timu yao kumaliza mzunguko wa kwanza ikiwa kileleni na pia imeweka rekodi ya kutopoteza mechi.**

"Hatukuwapokea wachezaji wetu tuliokuwa tunawasajili na kuwapeleka klabuni kwa bahati mbaya, ila ilikuwa ni kuwaweka kwenye misingi ya kutambua wanakuja kuitumikia timu yenye kiu na dhamira, timu kubwa yenye heshima, kwa hiyo hata hao wachezaji nao wamejikuta kwenye mshikamano na dhamira iliyopo, nao wakaingia kwenye malengo ya klabu," alisema Bumbuli.

Aliongeza mpaka sasa kuna baadhi ya vitu vimeonekana, ambavyo ni mshikamano mkubwa kati ya viongozi, benchi la ufundi, wachezaji, wadhamini, wanachama na mashabiki, lakini kuwa na kikosi kizuri kilichoboreshwa.

"Wote tumejikuta kwenye malengo na mikakati tulioiweka msimu huu kuwa tuwe na jambo letu," Bumbuli alisema.

Kuhusu kubadilisha benchi la ufundi, Bumbuli alikiri kuwa limewasaidia kufika hapo, lakini akadai kuwa lengo halikuwa hilo.

Mpaka sasa Yanga imemaliza mzunguko wa kwanza ikiwa na pointi 43, ikicheza mechi 17, ikishinda 13 na sare michezo minne.



Mshambuliaji wa Namungo FC, Steven Sey (kulia), akiwatoka wachezaji wa Al- Hilal Elobied ya Sudan katika mechi ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam hivi karibuni. Namungo ilishinda mabao 2-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Simba SC, Yanga zasubiriwa Zanzibar*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba wataanza kampeni ya kuwania ubingwa wa mashindano ya Kombe la Mapinduzi kwa kuivaa Chipukizi wakati Yanga yenyewe itashuka dimbani Januari 4, mwakani kupambana na Jamhuri kwenye Uwanja wa Amaan.

Akizungumza na visiwani hapa juzi jioni, Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano ya Kombe la Mapinduzi, Khamis Abdalla Said, alisema michuano hiyo mwaka huu itashirikisha timu tisa na zimepangwa katika makundi matatu.

Said alisema Kundi A linaundwa na Yanga, Namungo FC kutoka Tanzania Bara na Jamhuri ya Pemba wakati Simba, Mtibwa Sugar na Chipukizi ziko Kundi B, huku Azam FC, Malindi na Mlandege zenyewe ziko Kundi C.

"Timu tumezipanga katika makundi matatu ambazo zitacheza mechi mbili na kutoa mshindi mmoja na timu nyingine iliyofanya vyema zitasonga mbele na kucheza hatua ya nusu fainali," alisema Said.

Naye Katibu wa kamati hiyo, Imani Duwe, alisema bingwa wa michuano hiyo atapata kombe, Sh. milioni 15 na medali za dhahabu wakati mshindi wa pili atapewa Sh. milioni 10 na medali za fedha.

Hata hivyo alisema wanafikiria kutoa zawadi nyingine ya Mchezaji Bora endapo mchakato utakwenda vyema.

Aliongeza katika kuhakikisha wanadhibiti mapato, watatumia tiketi za mfumo wa elektroniki ambao utawabana wajanja wachache wenye tabia ya kutengeneza tiketi feki.

# Michezo

Jumamosi Desemba 26, 2020

Nipashe



Messi afichua siri kutong'ara LaLiga UKURASA 22



Wachezaji wa Azam FC, Awesu Awesu (kushoto) na Iddi Suleiman 'Nado', wakiwa katika mazoezi ya kujiandaa na mechi ya mashindano ya Kombe la FA dhidi ya Magereza itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

## Simba, Majimaji vitisho vyatawala

**Na Saada Akida**

WAKATI kikosi cha Simba kinarejea nchini leo kikitokea Harare, Zimbabwe walipokuwa na mchezo wa kimataifa wa Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Sven Vandenbroeck, amesema hawatakuwa na huruma kwenye mechi dhidi ya Majimaji kutoka Songea.

Simba ambao pia ni mabingwa watetezi wa mashindano ya Kombe la FA, wataikaribisha Majimaji katika mechi ya raundi ya tatu ya michuano hiyo itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini, Dar es Salaam.

Sven aliliambia gazeti hili akili, nguvu na mipango yao sasa inautizama mchezo huo wa Kombe la FA na amewataka wachezaji wake kuiweka 'kiporo' Platinum. Kocha huyo alisema wachezaji wake wako fiti kwa ajili ya kupambana kusaka matokeo mazuri na kila mpinzani watakayekutana naye watamheshimu.

"Hakuna mechi rahisi, tunarejea kwa ajili ya maandalizi ya mechi zijazo ikiwamo ya Kombe la FA, kikubwa wachezaji wako fiti kwa ajili ya kutafuta matokeo mazuri katika mechi hiyo," alisema Sven.

Naye Msemaji wa Majimaji, Godfrey Mvula, alisema wamejipanga vizuri na wamekuja Dar es Salaam kwa kazi moja ya kutafuta ushindi katika mechi hiyo.

Mvula alisema wanawaheshimu wapinzani wao, Simba kwa sababu ni mabingwa wa Tanzania hivyo wataingia uwanjani kwa tahadhari kutokana na kufahamu wametoka 'kujeruhiwa' na FC Platinum.

"Tumejipanga kuja kufanya kile walichofanya Mashujaa kipindi kile, tunahitaji kusonga mbele na kushiriki mashindano ya kimataifa mwakani kupitia njia hii, tumedhamiria kuiondoa Simba katika mashindano haya," alisema Mvula.

# Straika mpya kuipaisha Yanga

**Na Saada Akida**

## ●●● Kaze afunguka mazungumzo yafikia mwisho, nia ni kukamilisha malengo ya kutwaa...

HESHIMA imerudi! Hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, ambaye amesema yuko katika mchakato wa kusajili mshambuliaji mpya wa kimataifa kwa ajili ya kuimarisha kikosi chake kilichoko kwenye vita ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Mshambuliaji wa APR inayoshiriki Ligi Kuu Rwanda, Jacques Tuyisenge, anatajwa kuwindwa na Yanga ambayo awali ilionekana pia kuwania saini ya straika wa Plateua United ya Nigeria, Issa Ndala.**

Akizungumza na gazeti hili jijini, Dar es Salaam jana, Kaze alisema anaamini ujio wa nyota huyo mpya (hakutaja jina lake), ataongeza nguvu kwenye safu ya ushambuliaji kwa kushirikiana na Saido Ntibazonkiza ambaye 'makali' yake yameanza kuonekana.

Kaze alisema tayari amemkabidhi Ntibazonkiza jukumu la kufunga, huku akiweka wazi uamuzi wa kutua nchini mshambuliaji huyo mpya uko chini ya mabosi wa klabu hiyo.

Kocha huyo alisema anafahamu vyema uwezo wa Ntibazonkiza na ana imani nyota huyo ataendelea kutekeleza majukumu aliyopewa kama alivyofanya katika mechi mbili za ligi zilizopita ambazo Yanga ilipata idadi nzuri ya mabao ya kufunga.

"Kuna mabadiliko makubwa katika safu ya ushambuliaji, ujio wa Saido umesaidia timu yetu, lakini nimependekeza kupata mshambuliaji mwingine ambaye atakuja kuingia moja kwa moja kwenye kikosi cha kwanza na kazi yake kubwa itakuwa kufunga tu".

"Saido ni mzuri anajua kufunga ila jukumu lake sio hilo na akipata nafasi ya kufunga atafanya hivyo, nani anakuja hilo lipo kwa uongozi," alisema Kaze.

Aliongeza kwa sasa anawapongeza wachezaji wake kwa kumaliza mzunguko wa kwanza bila ya kupoteza mechi ana imani sio jambo rahisi katika ligi hiyo.

"Sio jambo la kawaida kumaliza mechi 17 bila kufungwa, hii ni juhudi za wachezaji wanapokuwa uwanjani, tunaenda kufanyia kazi upungufu wetu kwa ajili mechi zijazo," alisema Kaze.

Alisema pia wanahitaji kuimarisha kikosi cha timu hiyo, ili wafikie malengo yaliyotarajiwa na Wana-Yanga ikiwamo kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambao waliukosa kwa misimu mitatu mfululizo.

Naye Mkurugenzi wa Uendeshaji wa Kampuni ya GSM, ambao ni wadhamini wa Yanga, Hersi Said, aliliambia gazeti hili watatekeleza mapendekezo watakayopokea kutoka katika benchi la ufundi kwa kiwango cha asilimia 100.

Said alisema kila mchezaji atakayesajiliwa ndani ya kikosi cha Yanga atakuwa ni wa kiwango cha juu na ataingia moja kwa moja kwenye kikosi cha kwanza cha timu hiyo.

Baada ya mapumziko ya sikukuu ya Krismasi, kikosi cha Yanga ambacho kimeweka kambi jijini Mbeya kitaanza mazoezi leo kwa ajili ya kuwafuata Tanzania Prisons katika mechi ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa Desemba 30, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Nelson Mandela Mjini Sumbawanga.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >